**Utata** ukodishaji majengo Urafiki, mrithi NHC akana kutambua uhalali
UKURASA WA 4

**Wanaharakati**, waziri wakiri sheria ina shida kukabili ukatili wa kijinsia UK. 5




**Bodi** Mikopo Elimu Zambia yaja nchini kuchota uzoefu na maarifa HESLB
UKURASA WA 7

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatano Novemba 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581873

www.ippmedia.com

Nipashe Digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

**MOURINHO: RONALDO KUJA FENERBAHCE LABDA KUNYWA CHAI TU** UK. 22

# FUNGA KAZI

• **Vigogo** wahitimisha kampeni kila mmoja kwa staili yake, Rais Samia asema uamuzi wa wapigakura uheshimiwe... *Endelea Ukurasa 2*



Polisi Mkoa wa Songwe wakiwa katika doria za magari na miguu mjini Tunduma jana, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha ulinzi na usalama kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaofanyika leo. **PICHA: JESHI LA POLISI**

## Serikali yasitisha uokoaji Kariakoo, idadi ya waliofariki yafikia watu 29

UKURASA 3

## Dhuluma za mirathi zamshangaza waziri, waliolizwa wamjibu kwa ushuhuda mzito

UKURASA 3

**MICHEZO** **FADLU: TUTASHAMBULIA MWANZO MWISHO LEO** UK.24

**MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasalimia wananchi alipowasili katika mkutano wa kufunga kampeni za CCM uliofanyika uwanja wa Ujenzi wilayani Liwale, mkoani Lindi jana na kuhamasisha wananchi kupiga kura leo. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Funga kazi kwa vigogo wakihitimisha kampeni za uchaguzi serikali za mitaa

**Na Waandishi Wetu**

VIGOGO wa vyama vya siasa, jana walihitimisha kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika leo kwa staili tofauti kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Wakati kampeni hizo zikihitimishwa, Rais Samia Suluhu Hassan amewahakikishia wapigakura kuwa uamuzi wao utaheshimiwa.

Rais Samia amesema dhamira ya serikali ni kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa uwazi, haki na kwa kuzingatia kanuni za uchaguzi zilizoko.

Akizungumza jana na Watanzania kuhusiana na uchaguzi huo, alisema ni muhimu kuheshimu uamuzi wa wapigakura, kwa kuwa demokrasia yenye nguvu hujengwa kwa misingi ya heshima na mshikamano.

Rais aliwakumbusha viongozi wa vyama vya siasa, mawakala na wasimamizi wa uchaguzi kuzingatia na kuheshimu sheria na kanuni za uchaguzi ili uwe wa haki. Pia aliwakumbusha wasimamizi wa uchaguzi na wote wanaohusika na mchakato huo, kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa haki, uwazi na kuzingatia taratibu zilizokubaliwa na wadau.

Aidha, alitoa rai kwa kila mdau wa uchaguzi kutoa ushirikiano ili kufanikisha adhma ya kuwa na uchaguzi wa amani unaoakisi heshima kwa taifa lenye mshikamano na demokrasia imara.

Aliwakumbusha Watanzania kuwa kupigakura ni haki yao ya msingi, hivyo jukumu lao ni kuhakikisha wanaitumia kudumisha amani na utulivu na kujiepusha na vitendo vya uchochezi, vurugu au uvunjifu wa sheria.

Rais Samia alisema ni fursa muhimu kwa kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura kuchangia maendeleo ya nchi kwa njia ya kidemokrasia kwa kuchagua kiongozi mwenye sifa huku akiwasihi kujitokeza kwa wingi kupiga kura kwa kuwa ni fursa ya kuhakikisha uamuzi unaohusisha jamii unatokana na mahitaji halisi ya wananchi.

"Serikali za mitaa ni msingi wa ujenzi wa taifa imara na lenye maendeleo endelevu, kupitia viongozi tunaowachagua tunaweka misingi thabiti ya uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi na usimamizi wa rasilimali za umma," alisema.

**FUNGA KAZI**

Akifunga kampeni hizo zilizofanyika viwanja vya Liwale, mkoani Lindi jana, Waziri Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, aliwapigia debe wagombea wa chama hicho huku akisema kimechagua majembe ili kuwaletea Watanzania maendeleo.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, aliwaonya wagombea wa chama hicho watakaoshinda katika uchaguzi huo kutotumia madaraka yao kuwaumiza wananchi.

Alisema chama hakitakuwa na huruma kwa kiongozi wa namna hiyo na kwamba atachukuliwa hatua kali ikiwamo kutenguliwa. Alisema hayo jana wilayani Temeke katika Jimbo la Mbagala wakati akifunga kampeni za uchaguzi huo.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, John Mongella, akifunga kampeni hizo mkoani Shinyanga, aliwataka wananchi wa Shinyanga wachague wagombea kutoka CCM ambao ndio watawaletea maendeleo.

**CHADEMA TUMEPITIA MAPITO**

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrsia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, alisema: "Tumepitia mapito mengi katika uchaguzi huu. "Tumehangaika sana katika rufani. Hawa wagombea tulio nao tumeshinda majaribu kwa sababu hatukukata tamaa."

**Rais Samia alisema ni fursa muhimu kwa kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura kuchangia maendeleo ya nchi kwa njia ya kidemokrasia kwa kuchagua kiongozi mwenye sifa huku akiwasihi kujitokeza kwa wingi kupiga kura kwa kuwa ni fursa ya kuhakikisha uamuzi unaohusisha jamii unatokana na mahitaji halisi ya wananchi.**

Akifunga kampeni Ikungi mkoani Singida, Lissu alisema wamepitia mapito hayo bila sababu za msingi kwa kuwa watu waliopewa dhamana ya kuusimamia, hawakusimama vizuri katika nafasi zao.

Alisema licha ya chama kusimamia wagombea wengi, zaidi ya nusu wameenguliwa kwa sababu zisizo za msingi.

**ZITTO AFUNGUKA**

Kiongozi mstaafu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akifunga kampeni za chama hicho, alisema uchaguzi huo umeonesha ni kwa namna gani chama chao kimekua na kuimarika.

Alisema katika maeneo yote ambayo viongozi wakuu wa chama hicho walitawanyika, kote walisimamisha wagombea wenye nguvu na kwamba, wana uhakika wa kushinda leo.

"Mbegu mliyoipanda katika chama hiki imemea, imekua. Na imekua limtii likubwaa la Mlumba ambalo linaendelea kushamiri Jamhuri nzima ya Muungano. Watu wa Kigoma hongereni kwa kazi kubwa mliyoifanya," alisema.

**Inaendelea Uk.18**

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Dhuluma za mirathi zamshangaza waziri, waliolizwa wamjibu kwa ushuhuda mzito

**Na Elizabeth Zaya**

UJUMBE wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, kuhusu kuandika wosia wa urithi wa mali, umezua gumzo mitandaoni huku wengine wakishuhudia namna walivyokutwa na madhila kwa kukosekana wosia.

"Ndugu zangu, kwa dhati ya moyo wangu mkiwa wanandoa, kubalianeni muweke mambo yenu ya mirathi vizuri, siku moja mmoja kati yenu akitangulia mbele za haki, kusiwe na heka heka ya migogoro ya kesi na kuathiri watoto.

Na pia kwa upande wenu wanaume, nyie ndio viongozi wa familia na hususani pale penye ndoa, uelewa wenu na sauti yenu ni muhimu sana kwenye uongozi na maamuzi haya, tafadhali, toeni uongozi mapema kwenye ajenda hi muhimu," ulisomeka ujumbe wa Dk. Gwajima.

Alisisitiza mirathi hiyo inapaswa kuandikwa kwa walioooana au wasiooana isipokuwa kama wana watoto.

"Kama mmeoana na kuna watoto au hata bila watoto au hata kama hujaoa au kuolewa ila unao watoto, naomba andikeni mirathi yenu mapema kabisa ili mkitangulia au akitangulia mbele ya haki mmoja wenu wanandoa, msiache migogoro na kuacha watoto wenu kwenye mitihani. Tunapata changamoto sana kuhusu hizi kesi, mtakuja kukumbuka huu wosia.

"Kwa niliyoyasikia na kushuhudia katika kuhudumu kwenye hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuna kesi nyingi mno za migogoro isiyo ya lazima kuhusu mirathi, watoto wanahangaika wakati mwingine bila sababu.

"Ndugu zangu, dunia imeshajaa hila na husda na fitina na tamaa za mali, ambazo mtu hazimhusu na umdhaniaye siye, anakuja kuwa yeye kabisa. Watoto wanaumia, mzazi aliyebaki na watoto anaumia, ni vilio, na mara nyingi ni wanawake na watoto ndio wanaumia hapa. Uzuri kuna programu nyingi za msaada wa kisheria kuhusu hizi huduma, tutumie fursa hizi," aliandika Dk. Gwajima.

Baadhi ya watu walitoa maoni yao kwenye akaunti ya Dk. Gwajima akiwamo Mayenda Shabani, aliandika urithi utawafanya baadhi ya wanawake waanze kuua waume zao.

Rammy alisema: "Mama mbona kauli yako inalenga kwamba wanaume ndio tunatangulia kufa?"

Wakati Micho alisema mambo ya urithi yanachelewesha watu na kutaka kila mtu apambane mwenyewe.

Benny, alisema mali zake ataachia kanisa anakosali na kwamba mambo ya kurithisha mtu hapana.

Unique, alisema hasa wanaume ndio mali zao zote huandika majina ya mama zao.

Mrs Kayege alisema: "Mama umeniliza mimi, huu ujumbe umenigusa, yametukuta sisi kudhulumiwa haki zetu na baba mdogo kwa mambo kama haya hakika ushauri mzuri, asante mama."

Kiyenze alisema: "Sana mama yangu, ila huwa hawaelewi kabisa. Mimi najionea sasa, baada ya kifo cha marehemu mume wangu, napitia mengi, sasa familia imeshavurugika kabisa yaani inafikia hatua mke wa ndoa wanakukataa, cha kushukuru Mungu ni kwa kuwa kuna ndoa halali inasaidia, sasa ambao hawana ndoa sijui inakuaje...tujitahidi kuandika wosia ili kuepuka migogoro."

Vituko kitaani "Maandishi ya kisheria huwa yanadumu sana, maoni yangu urithi uandikwe maana ndio unabainisha kila kitu wazi."

Advocate Lorrayne aliandika: "Umetoa ushaui mzuri sana waziri, kuandika wosia sio uchuro bali ni kupanga mali zako zitumikaje, unapokuwa haupo tena duniani, sote ni wapitaji, lolote linaweza kutokea na popote ulipo na muda wowote na hasa familia zetu za kiafrika baadhi ya mila za desturi na dini.

"Tuna watoto kutoka kwenye mke zaidi ya mmoja ingawa hata wa mama mmoja nao pia wakati mwingine wanagombana. Lakini sasa sheria nazo kupitia maamuzi mbalimbali ya mahakama inaruhusu mtoto yeyote ili mradi upo ushahidi kuwa amezaliwa na baba wa mji basi naye ana haki, hilo nalo ni changamoto.

"Kwa kuwa wapo kinamama ambao wamechuma katika ndoa pamoja na inapotokea watoto ambao hawakutambulishwa kabla ya kifo cha mzee wa mji inakua changamoto, so na support kuwa tuseme na tuandike tu maelekezo yetu tukiwa hai."

Endendekisye aliandika: "Lakini mama haya masuala yanahitaji sana mwongozo wa wanasheria, asilimia 90 ya Watanzania elimu ya sheria imetupita kushoto, ombi langu kwako mama kabla ya hatujafikia uamuzi tunaomba sana elimu itolewe juu ya issue nzima ya mirathi."

Upendo Pallangyo alisema: "Mama umesema kweli tupu... Mume wangu alifariki 2021, tunasumbuana na ndugu zake vibaya mno, kesi ipo mahakamani... hili ni janga sana, nadhani ufanyike utaratibu iwe ni kama lazima kila familia ya mke na mume kwa ngazi ya familia na ukoo waambiane.

# Waliofariki dunia Kariakoo wafikia 29

**Na Halfani Chusi**

WAKATI serikali ikitangaza kusitisha ubomoaji na kutafuta watu katika ghorofa lililoporomoka Kariakoo, Dar es Salaam,Novemba 16, mwaka huu, idadi ya watu waliofariki dunia wamefikia 29.

Miili mitatu ya waliofariki dunia kati ya tisa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzuru eneo hilo, haijatambuliwa na watu wawili waliojeruhiwa katika ajali hiyo bado wanaendelea na matibabu.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, alisema jana kuwa hatua ya kubaini miili hiyo kwa njia ya vinasaba inaendelea.

Akiwa katika eneo hilo, Makoba alisema kazi ya uokozi na kuitafuta miili zaidi ya watu waliopoteza maisha imesimamishwa rasmi, hivyo kuruhusu wafanyabiashara kuendelea na shughuli zao kuanzia jana saa 8:00 mchana katika maeneo yote isipokuwa Mtaa wa Mchikichi.

Makoba ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), alisema baada ya kumaliza hatua ya uokoaji kinachoendelea ni kuondoa kifusi chote na kukihifadhi sehemu maalumu huku uchunguzi wa kubaini chanzo cha ajali ukiendelea.

Pia alisema jambo lingine linalofuata ni serikali kwa kushirikiana na wafanyabiashara kwenda kuzitambua mali zao ambazo zimehifadhiwa na zinalindwa na vyombo vya dola.

"Kamati ya maafa ya kitaifa ilipotokea maafa ilikuja kuweka kambi na sasa inakabidhi suala hilo kwa mamlaka za mkoa wa Dar es Salaam.

"Kwa hiyo upande wa mtaa wa Manyema na Mchikichi unaoishia Congo na Mchikichi (eneo ambalo ghorofa limeporomoka) utafungwa kwa siku mbili tatu wakati shughuli za uchunguzi zinaendelea. Mitaa mingine yote serikali imeamua ifunguliwe wafanyabiashara waendelee na shughuli zao kama kawaida," alisema Makoba.

Kuhusu wamiliki wa jengo hilo, alisema tayari wameshamtia nguvuni mmoja wa wamiliki na wengine wanaendelea kusakwa na Jeshi la Polisi huku uchunguzi ukiendelea.

"Kamati ya uchunguzi tayari imeshaanza kazi kwa hiyo tusiharibu uchunguzi," alisisitiza Makoba.

**SHANGWE WAFANYABIASHARA**

Mfanyabiashara wa Nguo Kariakoo, Remsi Mbilu, alisema kitendo cha serikali kuruhusu maduka yaliyokuwa yamefungwa yafunguliwe katika eneo yalikotokea maafa ni jambo zuri.

"Mfano mimi nilikuwa ninategemea biashara ili maisha yangu yaende, sasa kwa hizi siku kumi nilikuwa ninaishi kwa tabu sana," alisema.

Mfanyabiashara mwingine, Mahamudu Juma, alisema uamuzi wa kuwaruhusu waendelee na biashara una tija kwa kuwa maafa yameshatokea na kwamba huo ni mpango wa Mungu, hivyo lazima shughuli nyingine ziendelee.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Skani hapa kutembelea chaneli yetu



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na abiria alipokuwa safarini jana kutoka Dar es Salaam kuelekea mkoani Kigoma kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaofanyika leo, kwa ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Utata ukodishaji majengo Urafiki, mrithi NHC akana kutambua uhalali

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Wajasiriamali wa Chuma Chakavu (WCC-Beach Kidimbwi), kilichokuwa ndani ya eneo la Kiwanda cha Nguo cha Urafiki (FTC), Ubungo, Dar es Salaam, kimelalamikia kitendo cha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuwataka walipe kodi ya ardhi katika eneo la biashara ambalo walijenga vibanda kwa makubaliano na kiwanda.

Aidha, kimelitaka shirika hilo kutambua uwekezaji walioufanya kwa kujenga fremu za biashara 12 zilizogharimu Sh. milioni 159 kwa makubaliano na uongozi wa FTC ili wanufaike na uwekezaji huo.

Mei 17, 2024 kupitia vyombo vya habari, NHC iliutaarifu umma kuwa imenunua eneo hilo lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 50, kwa mnada wa wazi wenye thamani ya Shilingi bilioni tatu, ikijumuisha nyumba, maghala, viwanja vya wazi, viwanda na mali nyingine.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa chama hicho, Salum Abdallah, alisema walianza kuuza vifaa vya vyuma chakavu katika eneo hilo mwaka 2004 na sehemu kubwa ilikuwa ni bwawa la maji, lakini kwa uhusiano mzuri waliokuwa nao na Kiwanda cha Urafiki walitumia gharama zao kuziba eneo hilo hadi likawa rafiki kwa biashara.

Alisema kwa kuwa wafanyabiashara walikuwa na nia ya kufanya uwekezaji kwenye eneo hilo ambalo hapo awali lilikuwa na vibanda vidogo vya wafanyabiashara wa vyuma chakavu, uongozi wa Urafiki uliwashauri kuunda chama ili kuendeleza eneo hilo badala ya kufanya mtu mmoja mmoja, ndipo walipounda WCC.

Aprili 24, 2022 WCC iliomba kibali cha kufanya maboresho katika eneo hilo lenye ukubwa wa mita za mraba 177.4 iliyoko kwenye kiwanja namba 28456 kwa lengo la kuliendeleza na Julai 14, 2022 uongozi wa FTC uliwajibu kwa barua kuwa wameridhia ombi hilo kwa masharti ya kuwasilisha mchoro halisi wa ujenzi kabla ya kuanza utekelezaji na walifanya hivyo.

Alisema pia walifuatilia kibali kutoka Manispaa ya Ubungo cha kujenga ofisi za muda katika eneo hilo kama walivyokubaliana na FTC na ombi hilo liliokubaliwa kwa barua maalum Mei, 27, 2022.

Baaada ya kutimiza masharti chama hicho kilitumia akiba iliyopo kwenye akaunti yake ya benki Sh. milioni 159 na kujenga fremu za biashara 12 na kumaliza ujenzi Novemba 2023 na kuvipangisha Desemba, 2023.

Wakati wanajiandaa kuwasilisha taarifa ya gharama walizotumia kujenga katika eneo hilo kwa uongozi wa FTC, ili waingie makubaliano ya uwekezaji huo utadumu kwa muda gani kwa, uongozi wa kiwanda kiwanja hicho uliwataarifu wasubiri kwa kuwa eneo la kiwanda kwa sasa kipo chini ya NHC.

Alisema walishangaa Aprili 30, mwaka huu, shirika hilo bila kuzungumza na uongozi wa WCC waliwapelekea barua wapangaji waliowapangisha kwenye fremu walizojenga wakiwataarifu kuwa eneo hilo ni mali yao hivyo kodi ziwe zinalipwa NHC moja kwa moja.

"Wale wapangaji walishangaa na wakawaambia kuwa wanatambua fremu hizo ni mali ya WCC kwa sasa na ndio walioingia nao mkataba, lakini NHC wakawajibu kuwa hawatambui umiliki wetu sisi katika fremu hizo na kuwasisitiza kodi zote zilipwe kwao, jambo ambalo si sawa kwa sababu sisi tumewekeza pesa zetu na tumepangisha kwa miezi mitano tu na wao wakaingilia kati," alisema.

Waliandika barua makao makuu ya NHC kuwaomba watambue uwekezaji wao, wakati wakisubiri majibu mwezi Oktoba, NHC mkoa wa Ubungo uliwapelekea form za kusaini mkataba kati yao ambao ulikuwa na mabadiliko, ikiwamo kuwapandishia kodi ya ardhi kutoka Sh. 6000 kwa mita za mraba walizokuwa wanalipa hapo awali hadi Sh. 30,000.

Kwa mujibu wa Abdallah, walipokea fomu hiyo, lakini bado hawajatia saini na kuirudisha kwa sababu wanasubiri majibu ya madai yao waliyopeleka makao makuu.

Hata hivyo Novemba, mosi, mwaka huu NHC Ubungo iliwapelekea barua ya notisi ya siku 30 ikiwataka walipe deni la kodi ya ardhi ya Sh. milioni 14 .07 ikiwa ni sawa na Sh. milioni 1.698 kwa mwezi na ikiwa hawatekeleza agizo hilo mpaka Novemba 30, mwaka huu NHC itawavunjia mkataba.

"Tuliamua kulipa sehemu ya kodi hiyo kama Shilingi milioni tatu hivi, ili kushikilia wasivunje mkataba wakati tunasubiri majibu kutoka makao makuu juu ya uwekezaji tuliofanya katika eneo hili," alisema.

Katibu wa WCC, Festo Gabriel, alisema kuwa chama hicho hakina tatizo na kulipa kodi ya ardhi kwa kuwa ndicho walichokuwa wakifanya miaka yote wakati wapo chini ya FTC, wanachotaka wao ni uongozi wa NHC utambue uwekezaji walioufanya wa kujenga fremu 12 na wawaachie wanufaike.

**UONGOZI URAFIKI**

Meneja wa Kiwanda cha Urafiki, Thomas Mushi, amekiri kuwaruhusu WCC pamoja na wapangaji wengine kujenga fremu katika eneo hilo kwa makataba, lakini eneo hilo lilinunuliwa na NHC kwa mnada wa wazi na hafahamu sababu za shirika hilo kutotambua uwekezaji watu hao.

**NHC YAJIBU**

Meneja Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alisema baada ya kulichukua eneo hilo walilifanyia tathmini na kuwahakiki wapangaji wote waliokuwa chini ya Urafiki na kuwaweka chini yao ili wakubaliane na taratibu za upangaji wa shirika hilo.

Alisema wakati wanafanya tathmini waligundua kuwa eneo hilo lina thamani kubwa kinachohitajika kufanyika ni maboresho, ikiwamo kuondoa vibanda katika baadhi ya maeneo na kujenga nyumba za kisasa ili liendane na thamani. Alisema pia waligundua kuna vitu vingi vinaendelea ikiwamo watu kupangisha fremu kwa watu wengine na kupata faida zaidi jambo ambalo ni kinyume na taratibu za shirika hilo.

Alisema kwa upande wa WCC, shirika linatambua uwekezaji wao na limewapa eneo kubwa ambalo linatosha kufanyia shughuli zao na wanawatambua kuwa ni wapangaji wao, kama hawajaridhika na walichopewa wapeleke malalamiko yao kwenye shirika.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Aliyeshuhudia 'unga' atoa ushahidi kesi mume na mke

**Na Kulwa Mzee**

KOPLO Jackson Shambo (34) amedai alishuhudia unga uliokutwa nyumbani kwa mshtakiwa Samweli Kagisha na mkewe Brigitte Uwela ukifanyiwa uchunguzi na kubainika ni dawa za kulevya aina ya heroine.

Alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati akitoa ushahidi mbele ya Jaji Sedekia Kisanya.

Shahidi huyo alidai kuwa Januari 31 mwaka huu, akiwa ofisini, alipewa taarifa na kiongozi wake Inspekta Johari kwamba anatakiwa kushuhudia ufunguaji wa kielelezo.

Alidai alielekezwa baada ya kufungua na kukifunga, anatakiwa kupeleka kwa Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi.

Alidai alikwenda katika chumba cha kutunza vielelezo alikomkuta Inspekta Johari akiwa na washtakiwa wawili Samweli na Brigette, akaelekezwa kutafuta shahidi huru, alifanya hivyo akampata Julius Muzimu.

Alidai kuwa hatua ya kufungua kielelezo ilianza saa nane mchana ambapo Inspekta Johari alifungua bahasha ya kaki, ndani ikiwa na mfuko wa nailoni ang'avu ambao ndani yake mlikuwa na mfuko mweupe wa nguo ndani kukiwa na unga na chenga chenga zilizosadikiwa kuwa dawa za kulevya.

"Baada ya ufunguaji kukamilika, kielelezo kilifungwa, nilichukua na kukipeleka Ofisi ya Mkemia Mkuu, kilipokewa na Mkemia Emmanuel, niliongozana naye hadi maabara.

"Mkemia alichukua unga akaupima uzito, akapata gramu 978.42, alichukua sampuli kufanya uchunguzi wa awali, nilishuhudia uchunguzi maabara, baada ya uchunguzi aliniambia unga ule ni heroin," alidai.

Koplo huyo alidai alichukua sampuli nyingine kwa ajili ya uchunguzi zaidi na alimjulisha kwamba akimaliza ataandaa ripoti.

Alidai kuwa Februari 7 mwaka huu, alipigiwa simu kufuata ripoti ya uchunguzi.

Washtakiwa katika kesi hiyo wanadaiwa walikutwa na dawa hizo nyumbani kwao Shumbageni, wilayani Mkuranga.

Inadaiwa Januari 30 mwaka huu, Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa msiri kwamba watuhumiwa wanafanya biashara ya dawa za kulevya.

Baada ya kupewa taarifa hizo, inadaiwa askari wa jeshi hilo walifika nyumbani kwa watuhumiwa, wakafanya upekuzi na kukuta dawa hizo chumbani kwao.

HABARI KITAIFA

# Wanaharakati na waziri wakiri sheria ina shida kukabili ukatili

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) umeitaka serikali kufanya maboresho katika maeneo matano, ikiwamo Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, ili kusaidia kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia pamoja na kutunga sheria mahususi ya kupambana na vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa Mtandao huo, Dk. Monica Muhoja amesema kuwa muda uliobaki kufikia ukomo wa malengo ya maendeleo endelevu ni mfupi, hivyo kuna haja kuimarisha sheria na sera ambazo zitaharakisha ufikiwaji malengo ambayo nchi imejiwekea kutokomeza ukatili ifikapo mwaka 2030.

"Sisi wana-MKUKI tumefanya utafiti kubainisha upungufu kwenye Sheria ya Kanuni za Adhabu katika kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia.

"Tuko tayari kushirikiana ili tuwasilishe huo utafiti na tufanye tafakuri ya pamoja na wataalamu wa Wizara ya Katiba na Sheria ili kubainisha mikakati na maeneo ya maboresho.

"Pia tuko tayari kwa umoja wetu kuendelea kufanya kazi na wizara hiyo ili kuharakisha mchakato wa maboresho ya sheria hizo kwa sababu muda uliobaki wa kufikia mwisho wa malengo ya maendeleo endelevu ni mfupi," alisema Dk. Monica jijini Dar es Salalam juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya siku 16 za uanaharakati wa kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema eneo lingine ambalo waliomba ni mamlaka za usimamizi wa uchaguzi, kuandaa kanuni mahusus za utekelezaji kifungu cha 135 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani kuhusiana na masuala ya ukatili wa kijinsia kwenye uchaguzi.

"Hili limekuwa changamoto na kikwazo kikubwa katika ushiriki wa wanawake kwenye uchaguzi, hususani kwa wagombea, na tunataka liende sambamba na kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia wakati wa uchaguzi na siasa," alisema Dk. Monica.

Pia alisema wanataka serikali iimarishe utekelezaji Mpangokazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWA).

"Na hii kuanzia ngazi ya taifa mpaka vijiji na mitaa, tunaomba mamlaka husika zitenge fedha za kutosha kuwezesha utekelezaji mpango huu. Tunaomba mamlaka zote kushiriki kikamilifu kwenye vikao vya kamati ikiwamo kuwasilisha taarifa muhimu zinazohitajika kuimarisha uratibu na ushughulikiwaji changamoto mbalimbali," alisema Dk. Monica.

Wanaharakati hao pia walitaka masuala ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yajumuishwe katika ajenda za vikao vya ulinzi na usalama kwa ngazi zote.



"Pamoja na jitihada ambazo serikali inafanya kutokomeza vitendo vya ukatili, wanawake na watoto wengi wameendelea kuwa waathirika wa vitendo hivyo, pia kumekuwa na kulegalega kwa baadhi ya watendaji wa mamlaka husika katika kukabiliana na vitendo hivyo katika maeneo yao.

"Sisi tunaamini kwamba iwapo masuala hayo yakiingizwa katika ajenda za vikao vya ulinzi na usalama ngazi zote, kutaleta msukumo mkubwa wa uwajibikaji katika kushughulikia matukio ya ukatili," alisema Dk. Monica.

Pia waliomba serikali ifanyie maboresho sheria zinazogusa familia moja kwa moja ikiwamo Sheria ya Ndoa na na ile ya Mirathi.

"Kwa mfano, Sheria za Mirathi na Sheria ya Ndoa zinabagua sana wanawake na mabinti hususani wajane, hizi zinachangia wengi kupata matatizo ya afya ya akili kwa sababu wanakuwa wanakandamizwa sana. Kwa hiyo, tuko pamoja na serikali kushirikiana kuhakikisha vitendo hivi vinakomeshwa," alisema.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema vitendo vya ukatili ni aibu kwa nchi na havikubaliki, hivyo wizara yake iko tayari kukaa na wadau hao kupitia upungufu uliopo katika sheria mbalimbali zinazochangia vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Kwa mfano, Sheria ya Kanuni za Adhabu, ninashukuru kwamba mmefanya utafiti na kubainisha upungufu, nikiri kwamba ni kwa muda mrefu hatujafanyia maboresho katika eneo hili. Kuna haja tulifanyie kazi," alisema Prof. Kabudi.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701***

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UCHUKUZI

Simu : +255 (026) 2322703
Nukushi : +255 (026) 2322704
Baruapepe: km@uchukuzi.go.tz
Tovuti: https://www.uchukuzi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P 638,
40470 DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

### TANZANIA KUWA MWENYEJI WA MKUTANO MKUU WA SABA (7) WA JUMUIYA YA MAMLAKA ZA USIMAMIZI WA USAFIRI MAJINI AFRIKA

***Novemba 25, 2024 - Dodoma.***

Wizara ya Uchukuzi inautaarifu umma na wadau wa sekta ya usafiri majini kuwa Tanzania kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeteuliwa kuwa nchi mwenyeji wa Mkutano wa Saba (7) wa Kimataifa wa Jumuiya ya Mamlaka za Usimamizi wa Usafiri Majini Barani Afrika, utakaofanyika kuanzia tarehe 29 Novemba hadi 01 Desemba, 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Lengo la mkutano huu ni kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya udhibiti na usimamizi wa usalama wa usafiri majini barani Afrika huku kipaumbele kikiwa ni mustakabali wa usafiri wa majini na kuongeza ushirikano baina ya nchi wanachama.

Kauli mbiu ya mkutano huo ni **"Kuimarisha mustakabali wa sekta ya usafiri majini barani Afrika: Ushirikiano katika Teknolojia na Ubunifu ili kupunguza hewa ukaa, kuimarisha usalama, na mazingira ya sekta ya usafiri majini kwa mustakabali endelevu".**

Mkutano huo utatumika kama jukwaa muhimu katika kuwezesha wadau kushiriki katika majadiliano yanayogusa masuala ya teknolojia na ubunifu yenye kulenga katika kuimarisha usalama na mazingira ya usafiri majini, pia, watapata fursa ya kuingia makubaliano ya kibiashara pamoja na kuanzisha mitandao na ushirikiano katika uendeshaji masuala mbalimbali yanayohusiana na fursa za uchumi wa buluu.

Mkutano huu wa kihistoria utafunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na utahudhuriwa na Katibu Mkuu wa Shirika la Bahari Duniani (IMO), Bw. Antonio Dominguez pamoja na wataalam wa usafiri majini, viongozi wa mamlaka za udhibiti wa usafiri kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, zipatazo 50 ambazo zina bahari, maziwa na mito na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

Ushiriki wa Bw. Dominguez ni heshima kubwa kwa Tanzania hasa kipindi hiki tunapotekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu, ambapo kama nchi tumebainisha masuala ambayo Serikali kwa kushirikiana na wadau, kuhakikisha nchi inanufaika na fursa zitokanazo na rasilimali za Uchumi wa Buluu ili kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu.

Aidha, Tanzania itaendelea kutangaza fursa za kiuchumi zilizopo katika sekta ya usafiri kwa njia ya Maji zinazohusiana na utumiaji wa rasilimali za bahari na maziwa pamoja uchukuzi ili kukuza uchumi wa buluu, kufanya tafiti na kuwekeza katika uvunaji wa rasilimali bahari na maziwa zitakazosaidia kuongeza uwezo wa Serikali kuwahudumia wananchi na kuwaleta maendeleo endelevu.

Tunatoa wito kwa wadau wote wa sekta ya usafiri majini, wakiwemo wasafirishaji, wamiliki wa vyombo vya usafirishaji majini, wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, viongozi wa Serikali kujitokeza kwa wingi kuhudhuria mkutano huu muhimu ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha usafiri wa majini hapa nchini Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

Katika Mkutano huo pia kutakuwa na maonyesho na utoaji elimu kwa umma na washiriki watakao shiriki katika mkutano huo, hivyo tunawakaribisha wananchi wote.

**Imetolewa na:**

**Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb)**
**WAZIRI WA UCHUKUZI**

218265202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi Serikali za Mitaa ufanyike kwa amani, utulivu

**HAYAWI** hayawi yamekuwa. Siku iliyosubiriwa kwa hamu na wapenzi wa siasa, demokrasia na maendeleo imewadia. Ni siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambayo inawafanya wananchi kuamua nani awe kiongozi wao katika mitaa, vijiji na kuitongoji ili kushirikiana nao kutatua kero zinazowakabili.

Takribani vyama vyote vyenye usajili wa kudumu, vimefanya kampeni kwa wagombea viliowateua ili kuwawakilisha katika uchaguzi huo. Kwa mantiki hiyo, matokeo ya uchaguzi huo ni mavuno ambayo vitapata katika uwekezaji wa misingi ya sera na ahadi wakati wote wa kampeni.

Kwa mantiki hiyo, siku hii ya leo ndiyo ile itakayosadifu juu ya nini chama kitapata kwa kuchaguliwa au kutokuchaguliwa na wananchi. Kura zao ni matokeo ya sera na ahadi walizozitoa kwa wananchi.

Kwa ujumla, uchaguzi wa serikali za mitaa ni hatua muhimu kwa demokrasia na maendeleo ya wananchi kwa kuwa kama mchakato huo utaendeshwa kwa misingi ya uhuru na haki, watapata viongozi waliowataka ili kushirikiana nao kutatua kero zao kwenye maeneo husika.

Serikali za Mitaa ndilo chimbuko halisi la demokrasia na ni ngazi ambayo wananchi wanaweza kupanga, kuamua na kutekeleza mipango yao ya maendeleo. Kwa msingi huo, uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa ni mchakato muhimu katika kuwapata viongozi wenye upeo wa kushirikiana na wananchi katika kutambua kero zinazowahusu na kuzipatia ufumbuzi kupitia mipango watakayoamua.

Kutokana na umuhimu wa siku hii, Rais Samia Suluhu Hassan ametangaza kuwa siku ya mapumziko ili wananchi wapate fursa ya kupiga kura na kuacha visingizio kuwa hawakupata nafasi ya kuchagua viongozi wanaowataka. Kwa hiyo kila mwananchi aliyejiandikisha katika daftari la makazi, hana budi kutumia haki yake ya kidemokrasia katika kuchagua kiongozi anayemtaka kwa imani kuwa ndiye anayefaa kushirikiana nae katika kutatua matatizo yake.

Aidha, uchaguzi unatakiwa kuwa huru na wa haki, hivyo wadau wote kwa maana ya wasimamizi na wasimamizi wasaidizi, vyama vya siasa na vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kutenda haki ili viongozi watakaopatikana wawe wanaotokana na matakwa ya wananchi.


Maneno kama ushindi wa bao la mkono, kuingizwa masunduku ya kura zilizopigwa na kuingizwa kwenye vituo vya kuhesabia kura na watu kupewa ushindi isivyostahili ni sumu ya demokrasia. Kwa msingi huo, wasimamizi waache watu washinde kwa misingi ya kura walizopata na si kwa mahaba yao kwa chama fulani ili kuwasaidia watu kushinda tofauti na kinyume cha kura zilizopigwa.

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, kulitokea matatizo katika maeneo mbalimbali hata kufikia hatua ya kusema hakukuwa na uchaguzi bali uchafuzi. Kauli hiyo ililitia doa taifa na kuharibu taswira iliyojengeka kwamba Tanzania ni taifa la viwango vya juu katika dekomrasia na utawala bora na kujinasibu kwa misingi ya umoja, amani na mshikamano.

Kama Rais Samia alivyosema uchaguzi wa mwaka huu na ujao usilitie doa taifa, ni imani ya Watanzania na wapenda demokrasia duniani kote kuwa kauli hiyo ya kiongozi mkuu wa nchi itazingatiwa na mchakato huo kufanyika kwa misingi ya uhuru na haki. Vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kulinda amani na usalama badala ya kufuata maelekezo ya kundi fulani ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa misingi ya amani na utulivu. Kwa maneno mengine wasiwe chanzo cha kuharibu uchaguzi.

Tanzania yenye amani na utulivu, umoja na mshikamano inawezekana. Uchaguzi ufanyike kwa amani na taifa liendelee kwa ustawi na utengamano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tofautisheni vyeti na akili

Na Restuta James

**MWISHONI** mwa wiki iliyopita, gazeti hili liliandika ripoti maalumu ikionesha uhaba wa ajira kwenye sekta karibu zote, licha ya kwamba kila mwaka wanafunzi 100,000 wanahitimu vyuo vikuu.

Katika ripoti hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Ushirika cha Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUGECO), Revocatus Kimario, anasema kuna pengo kubwa kati ya ujuzi unaotolewa chuoni na ule unaohitajika kwenye ajira, hasa uthubutu na nidhamu ya kazi.

Anashauri kwamba badala ya wanafunzi kwenda kuzurura baada ya kumaliza vipindi, wachangamkie fursa inayoweza kuwafaa baada ya kuhitimu, akitoa mfano umuhimu wa kujifunza lugha mbalimbali za kimataifa.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa, anasema vyuoni wanatoa ujuzi wa aina tatu, unaohusisha uwezo kujua na kung'amua mambo, kutenda na mtizamo wa kuendelea kujifunza, akiwaomba wazazi na walezi wawajengee watoto maarifa hasa nidhamu ya kazi na kuheshimu muda.

Kwa muktadha huo ni kwamba, uhaba wa ajira ni tatizo moja, lakini nidhamu na weledi, kwa wale wanaofanikiwa kupata ajira ni tatizo jingine.

Ukizungumza na baadhi ya waajiri utabaini kwamba moja ya sifa wanayokosa wahitimu wengi wa ngazi mbalimbali vyuo vikuu, wana tamaa ya maisha, hawana adabu, weledi wala uwezo wa kutatua changamoto katika mazingira aliyopo yaani hapo kazini.

Mfanyakazi mmoja anayefanya kazi benki aliposoma ripoti ile aliniambia, tatizo sio ufaulu wa juu bali nidhamu.

Nidhamu inaanzia nyumbani hadi kwenye dunia ya teknolojia, hasa matumizi ya mitandao ya kijamii. Ni waajiri wachache wasioangalia akaunti za watu wanaowachagua kwenye usaili wa kazi.

Wengine wanaenda mbali zaidi kuangalia hata wale wanaoomba mafunzo ya vitendo (field), kujua aina ya mtu wanayempokea.

Ni jambo baya vijana wengi wanadhani wako huru kuamua nini cha kuposti kwenye mitandao yao ya kijamii, bila kupima madhara ya hicho kinachopostiwa.

Ni mbaya zaidi, ukiingia kwenye akaunti za mitandao ya kijamii ya hawa vijana, unakuta picha za starehe wengine wakivuta shisha na kumwagiana pombe.

Mabinti wakiwa nusu uchi kwenye fukwe, wakionesha maungo yao hata katika maeneo waliyopaswa kujisitiri. Kwa kifupi, ni vijana wanaoonesha kutaka maisha ya 'angani', ilihali uhalisia walipaswa kuwa wanafagia zizi la ng'ombe.

Kunywa na kustarehe wanajua, lakini hawawezi kutumia saa tatu kwa wiki kujifunza lugha ya kigeni, ambayo ingemfaa na kuiwezesha shahada yake kufanyakazi haraka.

Zipo taasisi zinazotafuta ajira za muda nje ya nchi, kuna nchi ili uweze kwenda lazima ujue lugha yao au ujue kuendesha gari. Sasa badala ya kujifunza hayo, kijana anajirusha akivuta shisha.

Kibaya zaidi ni kwamba baadhi yao hawataki kufundishwa wakiamini wameshafuzu kwa kufika chuo kikuu. Mathalani, ni kawaida kwao kumsikiliza mteja huku ameweka spika ya sikio (earphones), jambo ambalo halijengi mahusiano mazuri na mteja.

Kadhalika, wakikosea kazini wakiambiwa wanakasirika kwa kuwa wanaamini wanajua. Kwa kifupi ni vijana wasiopenda kuelekezwa wala kushauriwa. Ni hawa ambao wakiingia kazini, wanataka wamiliki magari mazuri na nyumba ndani ya muda mfupi.

Ripoti hiyo ya janga la ajira ilinikumbusha majibu ya Mwanafizikia Albert Einstein, alipoulizwa akili ni nini, akasema ni kile kinachobakia baada ya kuondoa yote uliyofundishwa darasani.

Kwa mujibu wa Einstein kuna watu wakiondoa yale waliyofundishwa darasani, vichwa vyao vinabaki vitupu. Hawa ndio hujisifia vyeti au idadi ya shahada walizonazo; akisema hawana akili, japo wana elimu.

Ninachotaka kusema ni kwamba wakati vyuo vikipitia mitaala na kuiboresha, vijana watafute kila mbinu ya kuwa wenye adabu, wenye kushirikiana na wengine, mwenye uwezo wa kushauri bila hila, ukarimu na utayari kujifunza kwa mkubwa na mdogo.

Inategemewa kwamba mtu aliye chuo kikuu, hapaswi kujiona mjanja akivuta shisha, bali analazimika kutambua madhara ya tumbaku na kuziepuka.



Wataalamu wa upasuaji wa moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), wakishirikiana na wenzao kutoka Shirika la Open Heart International (OHI) la Australia, kumfanyia upasuaji wa kurekebisha valvu ya moyo mgonjwa mwenye matatizo ya valvu wakati wa kambi maalumu ya siku 6 inayofanyika katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JKCI**

# Bodi Mikopo Elimu Zambia yaja kuchota uzoefu, maarifa HESLB

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) nchini imekaribisha timu ya maofisa sita kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Masomo (HESLB) ya Zambia kwa ziara ya mafunzo ya siku tano.

Jana katika ofisi za HESLB jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia alieleza furaha yake kuwa na timu hiyo ya Zambia kwa mara ya pili mwaka huu kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na maarifa.

Dk. Kiwia alionesha jinsi HESLB ilivyobadilisha uendeshaji na huduma zake kutoka mwongozo hadi kidigitali katika kipindi cha miaka 12 ili kuboresha utoaji huduma na usimamizi wa mikopo.

"Kabla ya mwaka 2012, shughuli zetu nyingi zilikuwa za mwongozo na karatasi nyingi... lakini tuliamua kukumbatia teknolojia na sasa hatuna karatasi," alisema Dk. Kiwia.

Mkurugenzi huyo pia alisema HESLB ambayo imetimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2004, imehudumia maelfu ya watanzania kupitia mikopo na sasa imejitanua na kuingiza mikopo kwa wanafunzi wa stashahada na inasimamia Ufadhili wa Samia, yaani Samia Scholarship.

"Mbali na mikopo, tunasimamia Ufadhili wa Samia kwa wanafunzi waliojiunga na Programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu.

"Hawa ni wanafunzi waliopata alama za juu katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita (ACSEE) katika tahasusi zinazozingatia sayansi," alisema Dk. Kiwia.

Mkuu wa ujumbe wa HELSB ya Zambia, Chiluba Kalungwana alipongeza alichokiita "kazi nzuri" inayofanywa na HESLB nchini na kusisitiza kuwa wao bado wachanga na kwamba kupitia ziara hiyo, timu inahitaji kujifunza kutoka HESLB jinsi ya kuboresha utoaji huduma zao na kujiinua kiteknolojia.

"Tunahitaji kujifunza jinsi tunavyoweza kujiinua kutoka kwa timu yako, tunaweza kuona ni maeneo gani tunaweza kuboresha," alisisitiza Kalungana.

Aliongeza, "Sisi sote ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashirika ya Ufadhili wa Elimu ya Juu (AAHEFA) na nchi nyingine nane zikiwamo Kenya, Uganda, Rwanda, Afrika Kusini, Malawi, Botswana, Lesotho, Namibia na Ghana."

HELSB ilianzishwa na Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Masomo ya Zambia Na. 31 ya Mwaka 2016, ikichukua nafasi ya Kamati ya Bursary ambayo ilianzishwa kwa Hati ya Kisheria Na. 182 ya 1973 ya Sheria ya Elimu, SURA 134 ya sheria za Zambia.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Container Space Solutions Tanzania Limited

Cheti cha Usajili Namba 118987

Sheria ya Makampuni, 2002

(KIFUNGU 334 (1))

MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha Container Space Solutions Tanzania Limited (kampuni), yenye usajili namba 118987, kilichofanyika tarehe 13 November 2024 azimio maalumu lilipitishwa:

1. Kufuatana na kifungu 331 (1) (b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. Wanahisa wamemteua Linda Allan Mwambete wa Mikumi House, 368 Msasani Road, Oysterbay, S.L.P 9673, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

.........................................

Linda Allan Mwambete

Mfilisi

wa Coffee Hub Company Limited

182709



**UBALOZI WA MAREKANI, DENMARK NA NORWAY DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Uingereza, Sweden na Helios Tower watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha, Magari na Majenereta tarehe 30 November, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa sets, Chest drawer, Draser, Mirror, Book shelves, Meza za Chakula, Viti, Makabati ya nguo,Vitanda, Magodoro, Steel lockers cabinet, Carpets, Fridge double door, Deep Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya Gas na Umeme, Meza za garden, Viti vya garden,Mashine za Photo copy Nashuatec MP6500, 5002, 2205 na Xerox 7970, Computer set, Laptops, Printer HP Laser Jet, Flat TV, A/c split unit, na vingine vingi.

**Magari na Majenereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Rover Discovery SE | SDV6 Diesel Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2011 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado S. Wagon | 1KZ Diesel Engine | 1994 | Umelipwa |
| 3 | Generator 33 KVA - 3 Phase | Perkins Diesel Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Generator 66 KVA - 3 Phase | Perkins Diesel Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Generator 150 KVA - 3 Phase | John Deer Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Generator 20 KVA - 3 Phase | Yanmar Diesel Engine | 2009 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 27 mpaka 29 November,2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Jenereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 6 December, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Jenereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA, Master cards na Lipa namba za CRDB yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

182710

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

# TAMWA yakemea udhalilishaji wanawake mitandao ya kijamii

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimesema kinaungana na Watanzania, wadau wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali kukemea vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na wasichana, hasa kupitia mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam, katika Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, zinazolenga kuikumbusha jamii kuachana na matendo ya ukatili, ikiwamo vipigo, ukeketaji, ubakaji, ulawiti, mimba za utotoni na rushwa ya ngono.

"Bado kuna changamoto zinazoibuka ambazo zinachagizwa na sheria mbalimbali, ambazo zina mapengo yanayochagiza ukatili wa jinsia na maendeleo ya kukua kwa teknolojia yameleta ongezeko kubwa la unyanyasaji wa kijinsia, kwa njia ya mitandao ya kijamii.

"Matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, imeathiri jamii hasa wanawake na wasichana ambao ndio mara nyingi wamekuwa walengwa wa picha zinazowadhalilisha," alisema.

Siku 16 zitahusisha tafakuri ya pamoja ya wapi palikofanikiwa, penye mapengo na ni kwa namna gani yatazibwa ili kupunguza ukatili wa kijinsia ndani ya jamii.

"Kaulimbiu ya maadhimisho haya kwa mwaka huu ni: Kuelekea miaka 30+ ya Beijing: Tuungane kumaliza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto'. Kaulimbiu hii inalenga kuwakumbusha viongozi, wanaharakati na wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia.

"Serikali, sekta binafsi, kampuni na wananchi kwa ujumla kuungana na kuchukua hatua, ili kumaliza ukatili kulingana na mapendekezo 12 ya mkutano wa Beijing, yaliyolenga kutokomeza vitendo vya ukatili wa jinsia na kukuza usawa," alisema Dk. Rose.

Alibainisha kuwapo mafanikio ikiwamo ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana-SOSPA na kuingizwa kwa kipengele cha rushwa ya ngono katika makosa yaliyo ndani ya Sheria ya Rushwa, pia nafasi ya mwanamke ngazi za uamuzi katika siasa imeendelea kuongezeka.

Dk. Rose alisema, wanawake wakiwamo wanasiasa wamekuwa wakidhalilishwa mitandaoni, hali inayochagiza kuacha kushiriki katika siasa au kutogombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye jamii.

"TAMWA, katika kipindi hiki cha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, ambacho kinaeandamana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Novemba 27, mwaka huu, tunakemea udhalilishaji wa wanawake kwa kutumia mitandao ya kijamii.

"Tunawahimiza wanawake na wasichana wanaogombea nafasi za uongozi katika uchaguzi huu, kuwa wastahimilivu, ili kutimiza malengo yao na wasiogope kutoa taarifa kwa mamlaka, pindi wanapodhalilishwa mitandaoni au kwa namna yoyote.



Wajasiriamali wa matunda wakipanga matikitimaji kwa ajili ya kuwauzia wateja wao katika Soko la Simu 2000 (Mawasiliano) Dar es Salaam jana ambapo tunda moja huuzwa kuanzia 1000 hadi 10,000 kulingana na ukubwa wake. Aidha wametaja kuwa msimu mzuri wa matunda hayo huwa ni kuanzia Februari. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CHADEMA yasisitiza wananchi kuchagua viongozi waadilifu

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

NAIBU Katibu Mkuu wa CHADEMA visiwani Zanzibar, Salum Mwalimu, amesema wananchi wanaweza kupata maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi katika maeneo yao iwapo watachagua viongozi waadilifu, watenda haki na wenye maono.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye viwanja vya Kapripointi mjini Mpanda mkoani Katavi, ikiwa ni siku za mwisho za kampeni za uchaguzi wa Serikali za mitaa zinazotarajiwa kufanyika leo nchini. "Viongozi wenye sifa hizo za kuwa na maono ya kiuongozi, uadilifu na watenda haki wapo Chadema hivyo wananchi wanapaswa kuwachagua viongozi hao ili waweze kuwaletea maendeleo endelevu kwenye maeneo yao," alisisitiza Mwalimu.

Alisema wananchi hawapaswi kudharau uchaguzi huo kwa kuwa unaweka viongozi muhimu, ambao kuna nyakati wanaamua mustakabali wa maisha ya wananchi wanaowaongoza na kwamba ni vema kushiriki uchaguzi huo na kuchagua viongozi sahihi.

Alitaka wagombea wa CHADEMA wanaoomba kuchaguliwa iwapo watapata nafasi za kuongoza mitaa, vitongoji na vijiji wasiige tabia za watangulizi wao waliotokana na CCM ambao walikuwa wakilalamikiwa kwa kujifanya ni miungu watu.

"Sisi CHADEMA viongozi wetu mahala popote wanasimamia misingi minne ya chama hiki, na yeyote anayekiuka misingi hiyo hatumuachi ya kwanza haki za watu, lazima tuwe na viongozi wanaosimamia haki za watu Mwenyekiti wa mtaa simamia haki za wananchi wako sio haki za wana CHADEMA haki za wananchi wote," alisisitiza.

Pia, alisema msingi mwingine ni uhuru wa wananchi, viongozi wanapaswa kutoa uhuru kwa wananchi kushauri na kuamua mambo yao, misingi mingine ni maendeleo ya watu na Demokrasia.

Awali, Mwenyekiti wa CHADEMA mkoa, Rhoda Kunchela alisema pamoja na kufanyiwa figisu katika mchakato mzima wa uchaguzi ikiwamo baadhi ya wagombea wao kuenguliwa, njia pekee ya wananchi kuiadhibu CCM ni kupitia sanduku la kura na kwamba wasisuse badala yake wajitokeze kupiga kura ili kupata viongozi sahihi wa kuongoza mitaa yao.

## 'Uchaguzi uwe fursa vijana kuchochea maendeleo'

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), Mohammed Kawaida amesema uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika leo, usiwe wa kupuuza, bali iwe ni fursa muhimu kwa kila Mtanzania hasa vijana kuonesha dhamira ya kweli ya kuleta maendeleo endelevu kwa taifa.

Aliyazungumza hayo jana mkoani Dar es Salaam, akisisitiza kwamba Watanzania wote wana wajibu wa kuhakikisha wanachagua viongozi waadilifu, wanaojali maslahi ya wananchi na wenye uwezo wa kusimamia maendeleo.

Alisema ni muhimu Watanzania kuchagua kiongozi ambaye wanaona anafaa katika kuleta maendeleo kwakuwa hiyo ndio demokrasia.

"Kuna sababu mbalimbali za msingi za kwanini, wananchi wanapaswa kuiunga mkono CCM katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa ikiwamo suala la kuona mafanikio ya kiuchumi.

"Mengine ni ustawi wa jamii kupitia miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imetekelezwa ikiwamo Reli ya Mwendo Kasi (SGR), Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), na uboreshaji wa bandari yamefungua fursa nyingi za ajira na kukuza uchumi wa ndani," alisema.

Aliongeza kuwa sababu nyingine ni utoaji wa huduma bora za kijamii, elimu na afya kwa wote, na chama hicho kimewekeza kwa kiasi kikubwa katika huduma za kijamii, ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora.

"CCM ni chaguo bora kwa Watanzania kutokana na historia yake, mafanikio na sera zake zinazojikita katika ustawi wa kila raia ambako kimewezesha utoaji wa elimu bila malipo, afya, majisafi na salama, uwezeshaji wa vijana, wanawake na wenye ulemavu huku kikitambua nafasi ya makundi yao katika maendeleo ya taifa," alisema.

Kawaida alisema katika uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu kwa wananchi kuendelea kuichagua CCM ili kuhakikisha mabadiliko hayo yanaendelea na miradi ya maendeleo inazidi kuwa na tija kwa jamii nzima.

Vile vile, alisema chama hicho kinatambua kuwa mafanikio ya serikali katika ngazi zote za kitaifa, yanategemea ufanisi wa viongozi wake na kwamba chama kimewekeza katika kuwaandaa na kuwajengea uwezo viongozi wake kupitia mafunzo ya uongozi na utendaji.

**"Kuna sababu mbalimbali za msingi za kwanini, wananchi wanapaswa kuiunga mkono CCM katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa ikiwamo suala la kuona mafanikio ya kiuchumi.**

# Wajigamba kumalizana leo na wasaka madaraka kwa rushwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WANANCHI eneo la Kwa Sadala Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wamesema 'amsha amsha' ya hamasa ya elimu ya mpigakura imewafungua macho ya namna ya kumalizana leo na wagombea wenye uchu wa madaraka na wanaotafuta uongozi kwa njia ya rushwa.

Wamesema elimu hiyo ambayo wameipata kupitia TUSONGE CDO kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji unaotarajia kufanyika leo, itawawezesha kumalizana na wagombea wa namna hiyo.

Akizungumza jana katika mkutano wa utoaji elimu ya mpigakura uliofanyika katika Soko la Kimataifa la Kwa Sadala, mfanyabiashara Allan Masacky, mkazi wa Bomang'ombe alisema:

"Hii hamasa inayofanywa na TUSONGE kuwaamsha wananchi kuchagua viongozi bora na kushiriki mikutano ya kampeni ni nzuri kwa sababu hatuwezi kuchagua viongozi mzigo wala rushwa wanaoshawishi wananchi kuwachagua kwa kuwapa fedha.

"Elimu tuliyoipata hapa ni namna bora ya kuwapata viongozi wa kidemokrasia, wanaotamani kuwajibika kwa ajili ya wananchi na watu wenye uadilifu katika jamii."

Gloria Tarimo, mfanyabiashara wa ndizi, alisema elimu ya kushiriki kupiga kura kumchagua kiongozi bora anayemtaka, amejifunza kwamba ni haki ya kila Mtanzania kupigakura kumchagua yule ambaye anafaa na kuwavusha katika gurudumu la maendeleo katika kijiji chao.

"Tumejifunza tunapaswa kuchagua mtu anayeweza kutatua changamoto zetu na kusikiliza wananchi wake wasema nini.

"Hatutachagua mtu ambaye anatumia nguvu ya fedha kuingia madarakani. Huyo ni lazima tujiulize kuna nini mpaka ananunua madaraka," alisema.

Erick Kitomary, fundi ujenzi na mkazi wa Kwa Sadala, alisema, "Nimevutiwa sana na ubunifu wa kampeni hizi za hamasa kuelekea uchaguzi hasa kwa namna wananchi walivyojitokeza kupata elimu ya mpigakura inayotolewa hapa.

"Nilichojifunza ni kuchagua mtu kutokana na sera yake ambayo amekuja nayo katika jamii, kwamba tunatakiwa kuzipima na kuchagua anayefaa, mwajibikaji na mtu mwenye hofu ya Mungu. Tunapaswa kuchagua kiongozi bora na si bora kiongozi," alisema.

Meneja Programu wa Shirika la TUSONGE CDO, Lawi Msemwa, alisema elimu ya mpigakura inatolewa katika eneo hilo kwa sababu vijiji vitatu vya Kwa Sadala, Mungushi na Kware vilivyoko Kata ya Masama Kusini, Wilaya ya Hai, mwaka 2020 vilionesha ushiriki hafifu katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Kwa mujibu wa Lawi, TUSONGE CDO inatekeleza hayo kupitia Mradi wa 'Maendeleo Yetu' unaofanywa kwa ubia, kati ya Shirika hilo na Taasisi ya Uwajibikaji wa Umma (WAJIBU), kuchochea ushiriki wa masuala ya utawala, uchaguzi, kupambana na ufisadi na rushwa.

"Elimu ya mpigakura tunayoitoa tunalenga kuboresha uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa raia katika uchaguzi huu na kuchochea mazingira ya uongozi na utawala unaowajibika," alisisitiza Lawi.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Kata ya Masama Kusini yenye Soko la Kwa Sadala, ina kaya 4,899 zenye watu 18,524, ambapo wanaume ni 9,063 na wanawake 9,461.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Tanga, Erasto Mhina (kulia), akifafanua jambo wiki iliyopita kabla ya kuingia katika kikao cha Baraza la Madiwani katika ukumbi wa Tate Plus. Wa pili kulia ni Diwani wa Kata ya Kisiwani, Shabani Chewaja, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Salimu Sechambo na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri, Luth Mwelo (kushoto). **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Padri ahamasisha kampeni za kistaarabu kulinda amani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

PAROKO Msaidizi wa Kanisa Katoliki Parokia Teule ya Utatu Mtakatifu Murombo, Padre Leon Ipoma, amewataka watu kufanya kampeni za kistaarabu, amani na utulivu, ili kuendelea kulinda amani iliyoko nchini.

Akizungumza jana wakati wa Misa Takatifu ya kuadhimisha Sherehe ya Kristu Mfalme, Padre Leon alisema ni vizuri viongozi waache wananchi wachague wanaowaona wanafaa kwa maendeleo.

Alisema ni vizuri kila mmoja akafanya kampeni kwa hali ya utulivu, hali ya amani sio kuvuruga amani ya nchi na sio wakati wa kufanya vita.

"Kristo Mfalme wetu ambaye leo tunasherehekea sikukuu yake sio mbaguzi na hivyo viongozi wa vyama vya siasa msichagulie watu viongozi mnaowataka nyie, waacheni wachague wale wanaowaona wanafaa kuwaongoza na kuwaletea maendeleo.

"Msishawishi watu kuchagua watu wasiowataka, 'eti wee unataka ashinde fulani' haifai na Mungu hapendi. Tuchaguwe viongozi wanaotoka kwa Mungu, kama Mungu amesema utakuwa kiongozi utakuwa tu, yule anayeonekana anafaa ndio wananchi wamchague," alisisitiza.

Tangu kuanza kwa kampeni hizo, Novemba 20 mwaka huu, jijini Arusha kumekuwa na shamra shamra za vyama mbalimbali vya siasa kufanya kampeni zao, huku magari, pikipiki mbalimbali zikipeperusha bendera zao.

**Akizungumza jana wakati wa Misa Takatifu ya kuadhimisha Sherehe ya Kristu Mfalme, Padre Leon alisema ni vizuri viongozi waache wananchi wachague wanaowaona wanafaa kwa maendeleo.**

# DC Simanjiro akabidhi gari jipya TAKUKURU

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Lulandala, ameikabidhi gari jipya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika kituo cha Mirerani kilichoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani humo.

Lulandala amekabidhi gari hilo jana kwa Kamanda wa TAKUKURU, Wilaya ya Simanjiro, Adam Mbwana, akiwa ndani ya ukuta unaozunguka machimbo ya madini ya Tanzanite na kuagiza kulitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kijiografia wilaya hiyo ina eneo kubwa la utawala, hivyo kwa kupatikana kwa gari hilo kutasaidia utendaji kazi kuwa bora zaidi hasa katika Tarafa ya Moipo.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa gari hili, kwa ajili ya matumizi ya TAKUKURU ukanda huu wa Tarafa ya Moipo kwenye suala la usafiri," alisema DC Lulandala.

Alisema kupitia gari hilo, watumishi wa taasisi wataweza kufika maeneo mbalimbali ya kata za Mirerani, Endiamtu, Naisinyai na Shambarai na kutoa elimu juu ya rushwa.

"Hapa Simanjiro tuna ofisi ya TAKUKURU inayohudumu Wilaya ya Simanjiro na makao makuu yake yako Mji Mdogo wa Orkesumet na hii iliyoko Tarafa ya Moipo ambayo ndiyo imepata gari," alisema Lulandala.

Kamanda wa TAKUKURU, Wilaya ya Simanjiro, Adam Mbwana, ameishukuru serikali kwa kuwapatia gari hilo.

Alisema kwa kutumia gari hilo, watafanya kazi zao kwa urahisi zaidi tofauti na awali ambapo kituo hicho hakikuwa na usafiri wa kuifuata jamii.

Kamanda wa TAKUKURU Mirerani, Sultan Ng'aladzi, alisema kupitia gari hilo, watakuwa na kitendea kazi kizuri cha kufanya kazi katika maeneo ya Tarafa ya Moipo.

"Hivi sasa hata kwenda kutoa elimu ya TAKUKURU Rafiki itakuwa rahisi kwa kuwa maeneo ya Kilombero au Lengasiti tutafikika na kutoa masomo mbalimbali ya kuzuia na kudhibiti rushwa," alisema.





# DC aagiza bodi kutoingilia majukumu ya kitaalamu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, ameitahadharisha Bodi ya Afya na Kamati ya Usimamizi ya Hospitali hiyo, kutoingilia majukumu ya wataalamu bali watekeleze wajibu wao kwa mujibu wa taratibu.

Kiongozi huyo alitoa agizo hilo juzi wakati akizindua bodi na kamati hizo na kuwataka wajumbe wake wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao, wasiingilie masuala ya kitaalamu, bali waulize kwanza taratibu zikoje, ili wazungumze lugha moja na kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

"Kazisome vizuri hizo nyaraka ili mjue majukumu yenu, na mfanye kazi vizuri ya uboreshaji wa huduma za afya, ili msijeingilia majukumu ya wataalamu," alisema Mtatiro.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, aliwasihi viongozi hao kusimamia ubora wa utoaji huduma za afya kwa wananchi.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Nuru Yunge, alisema wanayo hospitali moja, vituo vya afya vitano, na zahanati 44 ambavyo vinahudumia wakazi 468,611 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Alitaja majukumu ya bodi na kamati hiyo kuwa ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za afya, upatikanaji wa rasilimali na mgawanyo wake kwa kuzingatia mahitaji ya ngazi zote, kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato, itashirikiana na kamati za afya za vituo, sekta binafsi na wadau wengine, kwa nia ya kuinua kiwango cha afya na utoaji wa huduma.

Aidha, alisema bodi pia itawajibika kwa jamii katika kusimamia utoaji wa huduma bora za afya, upatikanaji wa dawa na vitendea kazi muhimu, pamoja na kuhakikisha kuna kuwapo na mahusiano mazuri kati ya watoa huduma na watumiaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Afya ya Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga, Adrian Joseph, aliomba ushirikiano ili kufanikisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi, huku akiwasihi wajumbe wa bodi kufanya kazi vizuri na wataalamu na siyo kutunishiana misuli.



Katibu wa Chemba ya Biashara ya Wanawake Kigoma- TWCC, Chichi Kamandwa, akitoa maoni yake kuhusiana na kodi ya mabango ya matangazo ya biashara wakati wa kongamano la kodi lililofanyika Kigoma. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Wanufaika TASAF wakusanya bilioni 8/- za kukopeshana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya vikundi 60,000 vya ujasiriamali vilivyoundwa na wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) vimekusanya Sh.bilioni 7.9 kwa ajili ya kukopeshana na kuepukana na mikopo umiza inayosababisha kuwarudisha nyuma kimaendeleo wanapoweka dhamana ya mali zao.

Mkurugenzi wa Mifumo na Mawasiliano kutoka Makao Makuu ya TASAF, Japhet Boaz, aliyabainisha haya katika kikao cha kujengwa uelewa viongozi na vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini na kusema, vikundi hivyo mpaka sasa vinawanachama 800,038 nchini nzima.

Alisema wanufaika TASAF wameweza kuunda vikundi vya ujasiriamali 60,342 na kujiwekea akiba ya Sh.bilioni 7.9 nchini nzima na kukopeshana Sh.bilioni 3.2 katika mzunguko wao kupeana na kurejesha na imewasaidia kuondokana na mikopo umiza iliyokuwa inawarudisha nyuma kimaendeleo hasa wanapoweka dhamana ya nyumba zao.

Boaz alisema kaya 84,674 zimefikiwa na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara na kusimamisha shughuli za kiuchumi zenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 31 na wataendelea kutoa elimu hiyo kila wanapowafikia, ili kuhakikisha walengwa wote wanaondokana na wimbi la umasikini uliokithiri.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Annamringi Macha, alisema baadhi ya wananchi hawaelewi namna TASAF ilivyoweza kukuza uchumi wa kaya na kuondokana na umasikini uliokithiri na kuwataka kuendelea kutoa elimu, ili kila mmoja wao atambue adhima ya serikali katika kupambana na janga la umaskini kwa wananchi wake.

Macha alivitaka vyombo vya habari kuendelea kuelimisha wananchi juu ya shughuli wanazozifanya walengwa na kupata ruzuku ili kuondoa tafsiri watu kuwa wanafanyishwa kazi kama wafungwa jambo ambalo sio kweli na ni sehemu moja wapo ya kujiingia kipato katika miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa.

Mmoja wa wanufaika hao, Rose Zakaria alisema waliamua kuanzisha mchezo wa hisa na kukopeshana ili kutojiingiza kwenye mikopo umiza ambayo inawafilisi na kuwarudisha nyuma kimaendeleo na wanakopeshana na kurejesha ndani ya siku 90 na kufanya hivyo ni sehemu ya kusaidiana wenyewe.

# RPC Kagera aahidi kulinda amani, utulivu

**Na Restuta Damian,**
KAGERA

KAMANDA wa Polisi mkoani Kagera, Blasius Chatanda, amesema amani na utulivu vitaendelea kutawala kabla na baada ya uchaguzi katika maneno yote yanayokaliwa na wananchi na hata barabarani.

Chatanda ametoa kauli hiyo wakati akipokea magari matano kutoka serikalini yaliyotolewa kwa ajili ya kufanya kazi siku ya uchaguzi na baada ikiwa ni kuboresha shughuli za jeshi hilo.

Chatanda alisema hakuna hali ya amani iliyopo na kuwataka watu wasisite kwenda kwenye maeneo ya kupiga kura bila kuhofia kuwa na mashaka ya kukosekana kwa amani.

Alisema mbali na uchaguzi ndani ya jeshi hilo kulikuwa na tatizo la vitendea kazi hasa upande wa magari, hivyo yaliyoongezeka yanategemewa kuongeza nguvu.

"Magari haya yamekuja wakati muafaka wakati ambao tutakikishia serikali kwamba tutawapatia wananchi amani ya uhakika kwenye uchaguzi na baada ya uchaguzi," alisema Chatanda.

Aliongeza amani hupatikana maneno yote hata katika barabara zilizoko mkoani hapa wapo wananchi wanaotumia vyombo vya moto na watembea kwa miguu, shughuli ya jeshi kitengo cha usalama barabarani kitakuwa kimeongeza vitendea kazi vipo.



Ukurasa 13

## UCHAGUZI S/MITAA WAPINZANI WAJA NA MKAKATI 'KUMSOMESHA MTU NAMBA'



Ukurasa 14

## DUMA BOKO ATIKISA

### Anatisha kwa mawaziri vijana yupo mwenye miaka 26

siasa
JUMATANO NOVEMBA 27, 2024
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

MAREKEBISHO SHERIA YA NDOA

# Watetezi wamshangaa waziri kuendeleza mfumo dume

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, kueleza kuwa kifungu kilichotumika katika kesi ya kubadilisha Sheria ya Ndoa ya 1971, siyo sahihi, wanaharakati wamshangaa kuendeleza mfumo dume.

Kesi ya kupinga umri wa ndoa, ilifunguliwa na Shirika la Msichana Initiative, ilipata ushindi kwenye mahakama ya rufani iliyoamuru vifungu 13 na 17 ambavyo vinaruhusu binti wa miaka 14 au 13 kuolewa, vifutwe.

Akichambua maelezo ya Waziri Kabudi, mwanasheria nguli na mtetezi wa haki za binadamu, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema mahakama ndiyo iliyotakiwa kusema kifungu hicho si sahihi na si mwingine.

Anaeleza kuwa kifungu cha 13 na 17 cha Sheria ya Ndoa ya 1971, kinafahamika na Mahakama ya Rufani na ndiyo iliyoelekeza kukifuta kama ingekuwa si sahihi isingefanya hivyo kwani ilikiona na kusikiliza hoja na kutoa maamuzi.

"Serikali iache visingizio na kuamua kwamba si sahihi mtoto chini ya miaka 15 kuolewa," anasema Dk. Hellen mwasisi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu -LHRC.

Wazo analosema Waziri Kabudi ni maoni yake kwa sababu kama ingekuwa hivyo, mahakama ilitakiwa itoe maoni hayo lakini imeona upungufu wa kisheria, hivyo wanatakiwa wakiondoe na si kupingana na chombo cha juu cha kutafsiri sheria na kulinda haki.

"Profesa Kabudi ni mwalimu wa sheria, kwenye familia ana msimamo kuwa tusome na tuangalie mambo ya anthropolojia ya



Mkurugenzi wa Taasisi ya Msichana Initiative, Rebeca Gyumi na DK. Ananilea Nkya (kulia), wakiwa katika moja ya matukio ya utetezi wa haki za kijamii. **PICHA: IPP**

sheria na tuunganishe na masuala ya jamii. Hili si suala la kijamii pekee , kwa sababu tiba za kisasa na utafiti, unaonesha kwamba mtoto akiolewa anaathirika na mengi," anasema Dk. Hellen.

Anthropolojia ni elimu inayochunguza maisha ya binadamu kwenye historia, ndani ya jamii, utamaduni, taratibu na hatua alizopitia na anazoendelea nazo hata sasa.

Anataja vifo vya mama na mtoto, fistula, matatizo ya afya ya akili, ulemavu wa nyonga na maradhi yasiyotibika kama saratani ya kizazi kuwa ni baadhi ya athari.

Anasema sheria haipaswi kuangalia anthropolojia na jamii, bali pia masuala ya afya na maisha ya binti anayeingia kwenye ndoa akiwa na umri mdogo.

Anasisitiza kwamba sheria irekebishwe kama hukumu ya Mahakama ya Rufani ilivyoelekeza, ili kuwa na jamii yenye afya timamu ya akili na mwili.

Mwanaharakati Dk. Ananilea Nkya, akizungumzia majibu ya Profesa Kabudi, kuhusu marekebisho ya sheria ya ndoa na hukumu ya Mahakama ya Rufani, anasema ameendelea kutetea mfumo dume unaowaminya haki watoto wa kike.

Anasema wakati mwingine kauli za viongozi kama hizo, zinawafanya wananchi waamini kuwa wanaosimamia watoto wao hawajali hatima zao, kwa sababu wanafamilia wa viongozi kama hao hawataathirika na ndoa au mimba za utotoni.

Anapinga maelezo ya Waziri Kabudi kwamba kulitakiwa kuwe na vifungu vya maelezo, maoni (commentary) kwenye katiba, akieleza kuwa kuna sheria zimerekebishwa ikiwamo ya mtoto ya 2009 ambayo haikugusa katiba.

Anamkumbusha Profesa Kabudi kuwa sheria ya makosa ya kujamiiana (1998) inayoharamisha pamoja na mambo mengine, ukeketaji na matendo ya ngono kwa watoto, ubakaji na ulawiti, na kutoa hukumu ya zaidi ya miaka 30 au maisha kwa wanaopatikana na hatia.

"Akumbuke ziliandikwa bila kuwekwa maoni ya kikatiba anayoyazungumzia. Ni mwanasheria na Waziri, mbona hazungumzii sheria ya uchaguzi na katiba inayokataza watoto wenye miaka 13 kupiga kura? Lakini mbona hawapewi mikopo benki? Inakuwaje waruhusiwe kuolewa?" Anahoji Ananilea.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, anasema kuendeleza mjadala ya kupinga marekebisho ya vifungu hivyo, kunaleta wasiwasi kwamba mfumo hauko tayari kuwalinda mabinti kwa kisingizio cha kusubiri marekebisho ya katiba.

Anasema huenda waziri hakubali mabadiliko kwa sababu ana uhakika watoto na wajukuu zake hawawezi kuingia kwenye ndoa hizo.

Anafafanua kuwa ndoa hizo ni matatizo yanayowapata watoto wa raia maskini, wasio na ufahamu na elimu, walio duni kiuchumi, wanaosoma shule za mbali, zisizo na mabweni, wala chakula na jamii inayowazunguka inanyanyasa watoto na kuendeleza mfumo dume na mila kandamizi, jambo ambalo halihusu familia za viongozi.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, akikosoa maoni ya Waziri Kabudi, anaeleza kuwa alitegemea serikali imetekeleza hukumu hiyo au kuomba mapitio ya hukumu, badala ya kuilalamikia mahakama.

Anamshauri Prof. Kabudi kuangalia hoja ya msingi ya haki za binadamu, ikiwamo ya mtoto kupata elimu, afya na kumiliki

INAENDELEA UK. 12

UCHAGUZI S/MITAA

# Wagombea wamemaliza kazi leo ni kupiga kura



Moja ya ofisi ya serikali za mitaa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**NA MWANDISHI WETU**

KAZI ya kuwasikiliza wagombea kwenye mikutano ya kampeni imemalizika, unapoamka leo kama umejiandikisha kupiga kura kuchagua viongozi wa serikali za mitaa ndiyo siku yenyewe ya kupiga kura yako, kwa hiyo wahi kituoni.

Ukumbuke uchaguzi wa serikali za mitaa mwingine, utafanyika 2029.

Mwananchi ulitakiwa kujiandikisha kwenye daftari la wakazi la mtaa mwezi uliopita, ili kuchagua kiongozi wa kijiji kama unaishi kijijini kadhalika na kitongoji lakini kwa wakazi wa mijini ni kuwachagua viongozi wa mitaa.

Uchaguzi huu unawahusu wananchi wa ngazi za chini ambao ndiyo wanaoutoa mamlaka kwa serikali zote za mitaa na ile kuu, mambo yakikamilika baada ya uchaguzi wa sasa wa serikali za mitaa kisha mkuu wa 2025 unaowachagua madiwani, wabunge, wawakilishi, marais na makamu wao.

Kama ulivyo uchaguzi mkuu, wa serikali za mitaa nao ni muhimu na umepewa umuhimu mkubwa, serikali ikitangaza rasmi kuwa leo ni siku ya kuwachagua viongozi kwa hiyo hakuna kazi za kiofisi ni mapumziko ili kila mmoja atumie wakati huo kupiga kura na kupunguza visingizio visivyo na sababu vya kutokuchagua viongozi wao mojawapo ikiwa kwenda kazini.

Wananchi wakumbuke kuwa vituo vya wapigakura vinafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni, hivyo waweke ratiba na kutumia haki yao ambayo ni kuwapata viongozi bora si bora viongozi.

Kumbukeni masuala mengi yanayohusu maendeleo yanaanzia kwenye ngazi za chini mfano vijijini, mitaani na vitongojini katika kipindi hiki ndiyo wakati wa kuangalia mbivu na mbichi kuchagua walio bora.

Mfano kuna viongozi ambao katika miaka mitano hawakuweza hata kuweka wavu kwenye madirisha ya ofisi za vijiji au serikali za mitaa wala kujenga vyoo, kuweka umeme au kuezeka ofisi, kuzikamilisha pale wenzao wa 2014 walioondoka 2019 walipoishia.

Ndiyo wakati wa wananchi kujihoji wanahitaji viongozi wa namna hiyo? Watu wasio watendaji wana sababu ya kuendelea kubaki ofisini? Ikumbukwe kiongozi anayetaka kuendeleza uzalendo wa tumbo na kusaka tonge kwenye maendeleo siyo mahala pake. Hivyo hahitajiki.

Kwa mfano huo ni lazima kuchagua viongozi wanaoweza kubadilisha fikira na kuleta maendeleo kama ambavyo wapo baadhi ya watu Goba jijini Dar es Salaam wamehamasisha wananchi kujenga vituo vya polisi, barabara za mitaa na kuboresha makazi yao.

Pamoja na kwamba si watendaji wa mitaa, lakini wamejaa hamasa ya kufikia maendeleo na maisha bora kwa wananchi.

Kwa baadhi ya wananchi miaka mitano wanakiri imekuwa michungu kama shubiri kutokana na kukosa huduma za kijimii lakini pia kukosekana viongozi wa kuwasemea na kutetea kwenye kuingizwa kwenye mipango ya maendeleo.

Kwa mfano kuna maeneo mengi jijini Dar es Salaam, watu wamekosa msaada mathalani wakazi wa Mbezi Msumi, eneo hilo linazungukwa na majirani kadhaa mfano Mbopo, Madale na Makabe. Ni sehemu zenye majisafi na salama, lakini Msumi wanakunywa ya mabondeni na kila uchao watoto na jamii ina maradhi ya maambukizi ya njia ya mkojo au UTI.

Wananchi wanashindwa kujua inakuwaje waishi kisiwani kwenye suala la maji wakati majirani wanaowazunguka wana maji ya kunywa safi na salama? Kadhalika Msumi sehemu ambayo ni karibu na Stendi ya Mbezi Magufuli haina barabara na hakuna kiongozi wa kuzungumzia kuikwangua na kuishindilia kwa katapila. Madaraja pia yamekatika ni kisiwa.

Tangu mwaka jana mwezi Desemba daraja maarufu la Kwa Ndee lilikatika na eneo hilo kukosa mawasiliano na Madale, Tegeta Nyuki na yeyote aliyetaka kupitia darajani hapo. Kwa miaka mingi ofisi ya serikali ya mtaa haina umeme hali imebakia hivyo kwa miaka mingi.

Wapigakura wa King'azi B, Dar es Salaam, nao walikuwa kwenye uongozi legelege kuanzia 2019 hadi sasa. Wanaeleza kuwa uongozi wa serikali za mitaa ulioondoka 2019, ulijenga ofisi kumaliza boma, kuliezeka, kuweka madirisha ya chuma (grill) na kuwa na ofisi.

Hata hivyo baada ya uchaguzi wa 2019 waliochaguliwa hawakufanya chochote kukamilisha ujenzi wananchi wakawa wanahudumiwa kwenye gofu, inakuwaje kwa uongozi kama huo?

Kuna visa vingi na masimulizi ya kila namna kuhusu uongozi wa serikali za mitaa kwenye miji mikubwa na midogo na vijiji pamoja na vitongojini.

Baadhi wanahusishwa na kuendeleza migogoro ya ardhi na wengine kuuza ardhi usiku ili wapewe hela au asilimia 10 ya gharama mnunuzi anazolipa.

Viongozi wa serikali za mitaa, baadhi wamekuwa lawamani kuwa wanachojitahidi hasa mijini na majijini ni kutafuta maslahi binafsi kama vile kuuza viwanja kwa wanunuzi zaidi ya mara mbili na wengine wakidaiwa kutishia mafundi wanaojenga 'saiti' na kuwalazimisha kusimamisha ujenzi ili wapate chochote kwa kutumia mgongo wa kukosa kibali cha ujenzi.

Viongozi kumbukeni kuongoza ni kuwa mtumishi wa wengine na siyo kujinufaisha kwa mambo ambayo hayana mifugo, lakini wakishindwa kufanikisha masuala ya usalama wa mali za wananchi kwenye kupambana na wahalifu.

Kuwapo kwa serikali za mitaa ni kufanikisha ugatuzi yaani kupeleka madaraka kwa wananchi na kufanyakazi kwa ukaribu zaidi na wana vijiji, vitongoni na mtaa kuanzia kutoa huduma, kupanga na kutekeleza mipango ya wananchi inayoandaliwa wilayani na kwenye serikali kuu.

## WATETEZI WAMSHANGAA WAZIRI KUENDELEZA MFUMO DUME

**INATOKA UK. 11**

uchumi.

"Serikali ingekata rufani kuomba mapitio ya ile hukumu kama waliona hayakuwa sawa kuliko kulalamika. Inatakiwa kuheshimu maamuzi hayo. Nasikitika kwamba hukumu inayokwenda kulinda na kutetea haki za mabinti zetu inaonekana siyo sahihi," anasema ole Ngurumwa.

Anasema mabinti wanaoolewa katika umri mdogo ndoa hazidumu na hivyo kuongeza mzunguko wa umaskini kwenye familia.

"Hata kama sheria zimekosewa tunapaswa kuangalia hoja ya msingi ya haki za binadamu kumlinda mtoto, kujenga kielimu na kiafya.

Katika mazingira ya kawaida, binti huyu anakwenda kuolewa ni dhahiri kwamba maisha yake na watoto wake yatakuwa magumu. Kama tuna lengo la kuondoa umasikini Tanzania, lazima tupige vita ndoa za utotoni," anasema ole Ngurumwa.

Mwanaharakati mtetezi wa haki za wasichana, Rebeca Gyumi, aliyefungua kesi hiyo mara kadhaa anasema ni muhimu iwepo sheria inayomtafsiri mtoto kiuhalisia bila kujali kama yuko shule au nje ya mfumo wa elimu, ili kuzuia ndoa za utotoni.

"Kuna mkanganyiko ndiyo maana tunatamani sheria ya ndoa irekebishwe kwa sababu mtu akimuoa mtoto chini ya miaka 18 ambaye ni mwanafunzi, anakabiliwa na hatia kwa mujibu wa sheria ya elimu. Lakini akiolewa binti wa miaka 14 aliye nje ya mfumo wa elimu inakuwa ni sawa. Hili ni tatizo," anasema.

"Inasikitisha mtu aliye chini ya miaka 18 haruhusiwi kuingia mkataba, kupiga kura wala kupewa leseni ya udereva lakini mtoto huyo anaruhusiwa kubeba jukumu la ndoa na familia," anahoji.

Rebecca anasema kifungu cha 13 na 17, kuruhusu binti aolewe akiwa na miaka 14, kinawaumiza zaidi watoto wa maskini wanaokabiliwa na changamato za maisha duni zinazowakwamisha kuendelea na shule.

Watoto wengi wanaoolewa katika umri mdogo wanalazimishwa na si ridhaa yao, kwani baadhi wanaelekezwa kufeli mitihani ili wasiendelee na shule.

Anatoa mfano wa Malawi, Bangladesh, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Zimbabwe zimeidhinisha kuwa umri wa kuoa na kuolewa ni miaka 18, anasema Rebecca.

Anasema baadhi ya nchi hizo zina idadi kubwa ya Waislamu.

Mkuu wa dawati la jinsia katika Kanda Maalamu ya Dar es Salaam, Leah Mbunda, anasema matukio mengi ya ukatili wa kijinsia yanatokea kwenye ndoa na kwamba walioolewa katika umri mdogo wananyanyaswa zaidi.

Imefika miaka mitano tangu Mahakama ya Rufani itoe tafsiri ya kisheria kuhusu umri wa mtoto kwamba ni aliye chini ya miaka 18, na kuielekeza serikali irekebishe sheria ya ndoa.

UCHAGUZI S/MITAA

# Wapinzani waja na mkakati ‘kumsomesha mtu namba’



Magdalena Sakaya



John Mnyika



Dorothy Semu

NA MWANDISHI WETU

LEO ni siku ya kupigakura kuchagua viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa baada ya wagombea kuhitimisha kampeni zao jana.

Ikumbukwe ni siku ya mapumziko na vituo vinafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 10 jioni, juu ya alama.

Tofauti na mwaka 2019, ambapo uchaguzi huo ulisusiwa, mwaka huu unashirikisha vyama 15 vyenye usajili wa kudumu ambavyo ni CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, CUF, NCCR- Mageuzi, Demokrasia Makini, UMD, NLD na DP.

Ni kwa mujibu wa Msimamizi wa Uchaguzi TAMISEMI, Ummy Wayayu, akiongeza pia kuwa vipo SAU, UPDP, UDP, AAFP na ADC.

Jana wagombea na viongozi wa vyama hivyo walikuwa wakinadi sera za vyama vyao kwa wananchi kwenye maeneo mbalimbali tayari kwa kuchaguliwa leo.

Hata hivyo, baadhi ya vyama vinaingia kwenye kinyang’anyiro hicho vikiwa na malalamiko ya kuenguliwa kwa baadhi ya wagombea wao katika vitongoji, vijiji na mitaa.

Pamoja na kuenguliwa, wapinzani wamekuja na mkakati ambao wanaamini utafanikisha kupata ushindi kwenye baadhi ya maeneo ambayo wagombea wao hawakuenguliwa au walienguliwa.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam, jana anasema pamoja na baadhi ya wagombea wao kuenguliwa hawajakata tamaa.

“Tumetoa maelekezo kwa viongozi wetu ambayo tunaamini bado chama chetu kitashinda na pia upinzani utashinda iwapo uchaguzi utaendeshwa kwa uhuru na haki,” anasema Dorothy.

Kiongozi wa chama anafafanua kuwa sehemu ambayo wagombea wao wameenguliwa, ACT-Wazalendo imeelekeza wanachama kupigia chama kingine cha upinzani chenye nguvu katika kitongoji, kijiji au mtaa.

“Hata kama atakuwapo mgombea mmoja wa upinzani asiye na nguvu, tutamuunga mkono tukiamini atashinda tu,

> “Tumetoa maelekezo kwa viongozi wetu ambayo tunaamini bado chama chetu kitashinda na pia upinzani utashinda iwapo uchaguzi utaendeshwa kwa uhuru na haki,” anasema Dorothy.

lakini kikubwa zaidi ni kwamba kule ambako wapo CCM pekee yao, tutawapigia kura ya hapana kwani hatuungi mkono wanaotaka ushindi wa mezani,” anasema.

Anaongeza kuwa huo ndio utaratibu wanaoingia nao kwenye uchaguzi wa serikali mwaka huu na kwamba kura za hapana zitaonyesha ni jinsi gani wananchi walivyochoka figisu za kuvuruga uchaguzi.

**MKONO WA CUF**

Naibu Katibu Mkuu CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema chama hicho kimetoa maelekezo kwa wanachama wake kupiga kura ya hapana kwa wagombea wa kijiji, kitongoji na mtaa ambalo wapinzani wameenguliwa.

“Tumetoa maelekezo hayo kwani maeneo mengi CCM imebaki pekee yake baada ya kuwaondoa wagombea wa upinzani. Nasi tumeona ni bora tufanye maamuzi hayo ili ikibidi uchaguzi urudiwe,” anasema Magdalena.

Anaongeza kuwa kama wangekuwa wanakubalika wasingetumia mbinu za kuengua upinzani ili wabaki pekee yao, na kwamba kitendo hicho kinaonyesha ni jinsi gani wanavyohofia uchaguzi huo.

“Nchi hii ni yetu sote na si kwamba CCM ndio wenye uwezo wa kuongoza kuliko wengine. Kama wanakubalika kwa nini watumie mbinu hizo kwa lengo la kupata ushindi bila jasho?,” Anahoji?

Magdalena anasema iwapo wanachama na wananchi wasio na vyama wakiamua kupiga kura za hapana kwa wagombea wanaotaka ushindi wa mezani, hatua hiyo itaonyesha ni jinsi gani wamechoshwa na mfumo uliopo.

Anasema wakati umefika kwa wananchi kuonyesha uamuzi wao kwa kuwachagua wale ambao wanawataka na kuwakataa wanaotaka kushinda kiulaini.

“Wananchi wasinyimwe uhuru wa kuchagua wagombea wanaowataka. Hivyo wito wangu kwao ni kwamba kila eneo ambalo wagombea wa upinzani wameenguliwa wapigiwe kura za hapana kwa sababu hakuna demokrasia,” anasema.

Katibu mkuu huyo anasema katika vitongoji, vijiji na mitaa, wananchi wa maeneo hayo ndio wanaowajua wale ambao wanafaa kuwa viongozi wao, kutaka wasilazimishwe kuchagua watu fulani.

“Inawezekana wenzetu wameamua kuziba masikio ili wasisikilize ya wananchi wanawataka kina nani wawaongoze, lakini ukweli ni kwamba msingi wote wa uongozi si uongozi tu bali uongozi bora unaoweza kuleta maendeleo unaanzia kwenye serikali ya mtaa ambako wananchi wanachagua bila kuingiliwa kwani wanawafahamu wanaofaa,” anasema.

**HADI KIELEWEKE**

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, anasema pamoja na changamoto za kuenguliwa kwa baadhi ya wagombea wao, wameamua kukomaa hadi kieleweke na leo wanashiriki katika uchaguzi huo.

Mnyika anasema wameamua kuendelea na uchaguzi huo tofauti na ule wa mwaka 2019 uliopa CCM ushindi wa asilimia 90 licha ya kwamba baadhi ya wagombea wao wameenguliwa bila makosa.

“Kwa mfano, kati ya vitongoji 64,274, tumeachiwa wagombea 14,805, lakini pia kati ya vijiji 12,333 tumeachiwa wagombea 4,175, huku mitaa 4,269 tukiwa tumeachiwa mitaa 2,686 tu,” anasema Mnyika.

Ni katika mkutano wake wa hivi karibuni na waandishi wa habari, mwenyekiti huyo anafafanua kuwa hata idadi hiyo ya wagombea wameipata baada ya kukomaa, vinginevyo wangeambulia wachache.

“Lakini pamoja na hayo, chama chetu hakijawahi kukubaliana kwa lolote kuhusu TAMISEMI kusimamia mchakato wa uchaguzi huo kuanzia uandikishaji ikiwamo ratiba ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kuwania uongozi wa mtaa,” anasema.

Anaongeza kuwa CHADEMA ‘inakomaa’ licha ya mchakato kuwa na changamoto kuanzia uandikishaji, kuchukua na kurejesha fomu hadi kuenguliwa au kuzuiliwa.

JUKWAA LA VIONGOZI

## DUMA BOKO ATIKISA

# Anatisha kwa mawaziri vijana yupo binti mwenye miaka 26



Rais mpya wa Botswana, Duma Boko.



'Miss World Africa' Lesego Chombo, Waziri wa Vijana na Masuala ya Jinsia. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

**Na Christina Mwakangale**

MWEZI huu wa Novemba kwa Botswana umeweka historia si kwa taifa hilo la kusini mwa Afrika pekee bali kwa bara zima.

Ni baada ya wananchi kusema 'noo' kwa chama tawala na kuunga mkono upinzani walioupigia kura za ushindi zikikiendea chama cha Umbrella for Democratic Change (UDC).

UDC ilipewa baraka kupitia kura za kuking'oa mamlakani chama tawala kilichodumu kwa takribani zaidi ya nusu karne kwa kupata kura za ushindi wa kishindo.

Chama tawala cha Botswana BDP, kilichokuwa kinaongozwa na rais aliyemaliza muda wake, Mokgweetsi Masisi, kilishindwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 30, mwaka huu.

Ushindi huo unahitimisha miaka 58 ya utawala wa chama hicho madarakani na kuongeza historia ya vyama tawala kwenye nchi zipatazo mbili barani humo kuondolewa madarakani na vijana majasiri wanaotoka vyama vya upinzani hivi karibuni.

Historia iliandikwa nchini Senegal taifa lililoko Afrika Magharibi linaloongozwa na rais kijana zaidi Bassirou Diomaye Faye (44) na sasa Botswana, inayoongozwa na Rais Duma Boko (54).

Botswana takribani asilimia 70 ya wakazi wake ambao ni milioni 2.3 ni vijana walio chini ya umri wa miaka 35, huku asilimia 70 ya idadi ya watu kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, umri wao ni chini ya miaka 30. Kwa upande mwingine, Faye, alishinda uchaguzi wa rais wa Senegal wakati Boko naye ameapishwa kuwa rais Botswana.

Taswira za viongozi hao zinatafsiriwa kwa namna tofauti na wachambuzi wa kisiasa kwamba ni viongozi vijana wanaokuja na mbinu tofauti kwa timu wanayoambatana nayo kuongoza wakiwachagua vijana wenzao.

Rais Boko wa Botswana, baraza lake la mawaziri alilolitangaza linakadiriwa takribani asilimia 45 ya mawaziri ni vijana.

> Kuna waziri kijana zaidi katika Baraza la Mawaziri la Rais Boko, binti Lesego Chombo, mwenye miaka 26 ambaye ni Waziri wa Vijana na Masuala ya Jinsia.

Kati ya mawaziri 18 miongoni mwao tisa umri wao ni chini ya miaka 50, kwa mujibu wa Shirika la Habari la Uturuki (TRT).

Wachambuzi wanaeleza kwamba hatua hiyo ni kuweka msisitizo wa kuwa na sura mpya za viongozi, kuendana na naye.

Kuna waziri kijana zaidi katika Baraza la Mawaziri la Rais Boko, binti Lesego Chombo, mwenye miaka 26 ambaye ni Waziri wa Vijana na Masuala ya Jinsia.

Chombo ni mwanasheria na mrembo akiwa Miss Botswana 2022 na pia ni 'Miss World Afrika 2024'.

Jacob Kalebeng (35), ni Waziri wa Michezo, akiwa na shahada ya sayansi ya siasa, huku Stephen Modise (37), ni Waziri wa Afya, lakini pia ni daktari wa binadamu na ana shahada nyingine katika elimu.

Bogolo Kenewendo (37), ni Waziri wa Madini, akitazamiwa kuimarisha uchumi kupitia sekta hiyo hasa madini waliyonayo nchini humo ambayo ni almasi.

Kenewendo ana shahada ya uzamili katika uchumi wa kimataifa, kutoka chuo kikuu cha Sussex cha Uingereza na shahada ya uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Botswana.

Waziri wa Serikali za Mitaa na Masuala ya Utamaduni ni Ketlhalefile Motshegwa (40), ana shahada ya sayansi ya jamii na ya uzamili katika viwanda, ajira na uhusiano.

Kadhalika Rais Boko, amemteua Phenyo Butale (44), kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, ambaye ana taaluma ya lugha na ana shahada ya uzamivu-PhD katika eneo hilo pia.

Kwenye Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji, ni Noah Salakae (47), elimu yake ni mhandisi na meneja miradi huku David Tsher ana umri usiozidi miaka 50, akiteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Ubunifu.

Ana shahada ya sayansi na masuala ya uhandisi tiba kutoka Chuo Kikuu cha US, huko Marekani. Pia Makamu wa Rais Ndaba Gaolathe (52) ana shahada katika hisabati na nyingine ni kwenye utawala, biashara, uchumi na sheria.

Waziri wa Sheria na Masuala ya Kubadilisha Mwenendo ana miaka 54 naye ni Nelson Ramaotwsana akiwa na shahada ya uzamili ya sheria.

Waziri wa Ofisi ya Rais, Moeti Mohwasa (55), ana shahada na ni mhariri wa habari.

**RAIS BOKO**

Rais Boko, amebobea kwenye haki za binadamu na ni wakili. Elimu yake ya uanasheria ilianzia nchini mwake, hatimaye kwenda Shule Kuu ya Sheria ya Harvard, huko Marekani.

Kwa miaka 50 wapinzani wa kisiasa nchini humo, wamekuwa wakiota ndoto, kukivua madaraka chama kikuu cha BDP, lakini ni Boko pekee ndiye aliyefanikisha hilo.

Mbinu ya ushindi wa chama chake cha Umbrella for Democratic Change ilishangaza. Yeye mwenyewe Boko, amekiri kushtushwa na idadi hiyo ya kura za ushindi.

"Ninaweza tu kuahidi (kwa watu) nitafanya kila niwezalo. Nitakaposhindwa, nitawatazama wao, waniongoze."

Katika muda wote wa kampeni yake, mikutano ya hadhara, Boko alikuwa akiwaomba wafuasi wake kuja karibu na kuwasikiliza malalamiko ya wapigakura njia ambayo ilimfanya kuwavutia vijana.

Akizaliwa mwaka 1969, katika wilaya ya kati nchini humo, katika mji mdogo wa Mahalapye. Boko daima alikuwa na hisia ya heshima, kulingana na marafiki.

Wakati wa shule, alichaguliwa kuwa rais wa baraza la wanafunzi, wakati kwenye taaluma ya sheria, aliibuka kuwa mmoja wa wanasheria wakuu nchini, kulingana na mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Lesole Machacha.

Ushindi wa upinzani nchini humo ambao haukutarajiwa ni pigo kubwa la chama tawala na Masisi aliyeingia madarakani mwaka 2018. Chama chake kimekuwa madarakani tangu Botswana ilipopata uhuru kutoka kwa Uingereza, mnamo mwaka 1966.

***MITANDAO***



# Serikali yaipatia TIA bilioni 13/- ujenzi majengo ya taaluma

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SERIKALI imepatia Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida, Sh. bilioni 13.5 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya taaluma ili kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na taasisi hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Prof. William Pallangyo, alibainisha hayo juzi wakati wa mahafali ya 22 yaliyowahusisha wahitimu 1,477 wa kampasi hiyo.

Alisema kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga katika taasisi hiyo ambapo katika mwaka wa masomo 2024/25 wamelenga kudahili wanafunzi 1,600 na hadi sasa wameshadahiliwa 1,276.

Prof. Pallangyo alisema kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kumetokana na utaratibu wa serikali kupitia TAMISEMI kuwapangia vyuo wahitimu wa kidato cha nne, ongezeko la wanufaika wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), kuanzishwa kwa shahada ya uzamili na ubora wa elimu unaozingatia umahiri wa mafunzo kwa vitendo.

Aidha, alisema taasisi hiyo imeandaa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 52 kuhusu usimamizi wa fedha za umma, utawala bora na uongozi ambapo kampasi ya Singida imeendesha madarasa ya maandalizi ya mitihani ya Bodi ya Uhasibu (CPA) na Bodi ya Ununuzi na Ugavi (CSP).

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliwataka wahitimu kupenda kujiajiri hasa katika kipindi hiki ambacho taifa limeweka mazingira mazuri ya vijana kupata mitaji bila riba yoyote.

Dendego aliwasihi wahitimu kutumia mitandao ya kijamii kama jukwaa la kutangaza bunifu zao kwa kukutana na wateja na kueneza mawazo mapya ya kuliendeleza Taifa badala ya kupoteza muda mwingi kwenye mitandao kwa kujadili mambo yasiyo na manufaa.

Mjumbe wa Bodi ya Kiushauri Wizara ya Fedha, Renatus Msangira, alisema TIA kampasi ya Singida inatoa mafunzo kwa ufanisi na ushindani na kufanya tafiti zenye manufaa kwa jamii na nchi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika fani za uhasibu, ugavi na nyingine.

# Wizara yaagiza wathibiti ubora kuzisaidia taasisi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Wilson Mahera, amewataka wathibiti ubora wa shule kuzisaidia taasisi wanazozifanyia tathmini kufikia viwango vya ubora vilivyowekwa nchini, ili kuleta ufanisi kwenye mageuzi ya elimu.

Dk. Mahera aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo elekezi ya siku tatu kwa maofisa uthibiti ubora wa wilaya wateule yenye kaulimbiu isemayo 'Uthibiti Ubora wa Shule unaozingatia weledi, maadili na uwajibikaji kwa matokeo chanya ya ujifunzaji'.

Aidha, alisema uthibiti ubora wa shule ni chombo muhimu cha kutathmini ufanisi wa shule na vyuo vya ualimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

"Hivyo wajibu huu unawataka wathibiti ubora kuzisaidia taasisi wanazozifanyia tathmini kufikia viwango vya ubora vilivyowekwa na nchi, na ni muhimu sana kujiongezea ujuzi na maarifa kila wakati pengine pasipo kusubiri mafunzo kama hayo kutokana na upatikanaji wa rasilimali fedha," alisema.

Aidha, aliwaasa maofisa hao kutumia fedha kidogo walizonazo kuleta matokeo kwa kuwa serikali inategemea matokeo zaidi kutoka kwao.

"Nimefahamishwa kwamba mmejifunza mambo mengi katika mafunzo haya ambayo ni pamoja na wajibu wenu katika usimamizi wa utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa; Maeneo muhimu ya Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule yaliyoboreshwa kulingana na mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya elimu," alisema.

**Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, Ephraim Simbeye, alisema Wizara ya Elimu kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, imetekeleza maboresho ya muundo wa Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na kwa sasa muundo unawatambua maofisa hao wa wilaya.**

Alisema pia wamefundishwa kuhusu mfumo wa uthibiti ubora wa shule, muundo wake na namna utakavyotumika pale utakapokuwa tayari; taratibu za manunuzi ya umma kwa kutumia mfumo wa NeST, matumizi ya mfumo wa usajili wa shule (SAS), masuala ya taratibu za fedha, masuala ya sheria ya elimu na yahusuyo utawala na uendeshaji wa ofisi zao.

"Ni vema kuwa na jitihada binafsi za kujiongezea maarifa kupitia fursa nyingine za kutumia kwa manufaa maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani na ya mitandao mbalimbali," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, Ephraim Simbeye, alisema Wizara ya Elimu kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, imetekeleza maboresho ya muundo wa Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na kwa sasa muundo unawatambua maofisa hao wa wilaya.

Alisema kutokana na maboresho ya mitaala ya elimumsingi, wizara imeboresha Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule cha Mwaka 2017 na miongozo yake ili viendane na matakwa ya mitaala.



Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaafa Rajabu, akiwaonesha mashekhe, maimamu na walimu wa madrasa (hawapo pichani), tuzo aliyokabidhiwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), baada ya kutunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima (PhD) iliyotolewa kwa udhamini wa Outreach Care International kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Cornerstone International College - USA, Lucent University - UK na HHWB College – USA jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC Dodoma aonya vijana kutumiwa na wanasiasa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

IKIWA leo ni siku ya uchaguzi wa serikali za mitaa, vijana mkoani Dodoma wametakiwa kujiepusha kutumiwa na wanasiasa kufanya vurugu kwa maslahi yao na kutanguliza uzalendo wa taifa lao.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mdahalo wa vijana kutoka vyuo vikuu na vya kati ulioandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo.

Senyamule alisema vijana kulinda amani na utulivu uliopo na wasikubali kurubuniwa au kushawishiwa na wanasiasa kuleta vurugu katika uchaguzi huo.

Aidha, alisema katika mdahalo huo vijana wamejadili masuala ya ukosefu wa uzalendo unachochea ushiriki hafifu katika uchaguzi hivyo na kuwataka vijana kuwa wazalendo kujitokeza kupiga kura kwenye uchaguzi huo kwa amani.

Naye Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Victor Swella, alisema vijana wanapaswa kutambua athari za mmomonyoko wa maadili unatokana na vitendo vya kukosa uzalendo katika jamii, ambavyo vinachangia vitendo vya rushwa.

Aidha, aliwataka vijana kupitia midahalo inayofanywa na TAKUKURU itumike kujifunza kupeuka masuala ya kushawishiwa kufanya vitendo viovu ambavyo vinapelekea kuchochea rushwa katika kizazi hiko ambacho ni taifa la kesho.

"Kupitia hii midahalo mnapaswa kuwa mabalozi wazuri katika suala la kupiga vita rushwa katika maeneo mnayotoka, msaidie kutoa elimu kwa vijana wenzenu ambao hawajabahatika kuhudhuria midahalo," alisema Swella.

Kadhalika, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema vijana wanaotambua nini maana ya uzalendo hawawezi kuleta vurugu kuelekea uchaguzi katika serikali za mitaa, isipokuwa watafuata taratibu ili kupiga kura kwenye uchaguzi huo.



# TFS yatoa mabati ujenzi Kituo cha Polisi Igoma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kupitia shamba la miti la Kiwira mkoani Mbeya, umetoa msaada wa mabati 96 kwa ajili ya kuezeka Kituo cha Polisi cha Igoma, ambacho kinajengwa kwa nguvu za wananchi.

Msaada huo ulitolewa juzi, ikiwa ni sehemu ya mchango wa TFS kwa jamii inayozunguka shamba hilo, wenye lengo la kutambua ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na shamba hilo kwa ujumla.

Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Kiwira, Thadeus Shirima, akikabidhi mabati hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, alisema uongozi wa TFS umeamua kutoa msaada huo, ili kuunga mkono jitihada za wananchi.

Shirima alisema kituo hicho kipo jirani na shamba la miti la Kiwira, hivyo kama sehemu ya jamii wameamua kushiriki katika ujenzi huo kwa kutoa mchango huo wa mabati.

"Wananchi wanaoishi kuzunguka shamba letu, ni watu ambao tunashirikiana katika ulinzi wa misitu na rasilimali nyingine zilizo ndani ya shamba hili, hivyo kwa kutambua mchango wao, tumeamua kuwaunga mkono katika ujenzi wa kituo cha polisi.

"Kama sehemu ya jamii, tunaamini tutanufaika na uwapo wa kituo hiki cha polisi, hivyo nasi tumejisikia kutoa mchango wetu kama wanufaika," alisema Shirima.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa, alisema kituo hicho kitasaidia kuimarisha usalama wa wananchi katika eneo hilo na kata za jirani, ambako kuna shughuli nyingi za kiuchumi zinafanyika.

"Wananchi wa eneo hili ni wakulima wazuri wa viazi mviringo na mazao mengine ya kibiashara, lakini pia kuna shamba la miti la serikali na ya watu binafsi.

"Kutokana na shughuli hizi za kiuchumi, eneo hili lina mwingiliano mkubwa wa watu, hali ambayo inasababisha kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa kituo cha polisi kwa ajili ya kuimarisha usalama," alisema Malisa.

Alisema uwapo wa kituo hicho, utasaidia kupunguza matukio ya uhalifu katika mazingira ikiwamo udhibiti matukio ya uchomaji moto misitu.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Igoma, Andrew Mwaipopo, alisema wananchi wa kata hiyo wanatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo bado wanahitaji misaada zaidi kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.

Alisema mbali na ujenzi huo, wananchi wa kata hiyo pia, wanajenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), ambacho baadhi ya majengo yake yamefikia hatua ya kupaua na hivyo, kuomba wadau zaidi kujitokeza kuwasaidia.

Alisema katika kata yake pia, kuna ujenzi wa kituo cha afya ambao unaendelea ambapo ukikamilika utakuwa na msaada mkubwa katika maendeleo ya wananchi wake na wale wa maeneo ya jirani.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (kulia), akipokea moja ya mabati kutoka kwa Mhifadhi Mwandamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Thadeus Shirima, juzi ambaye ni Mkuu wa Shamba la Miti Kiwira, mabati hayo ni kwa ajili ya kuezekea Kituo cha Polisi cha Igoma wilayani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CHAUMA yajinadi kukabiliana na mmomonyoko wa maadili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) Mkoa wa Mbeya kimeahidi kusimamia tatizo la mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii endapo wananchi watawachagua wagombea wake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika leo nchini.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akinadi sera za chama chake mtaani, Mwenyekiti wa chama hicho mkoa, Ipyana Njiku, alisema kipaumbele chao ni suala la maadili kwa sababu viongozi wa serikali za mitaa wana nafasi ya kubadilisha jamii katika hilo.

Njiku alisema baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa wamekuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili, kwa kuwa sehemu ya kuficha vitendo viovu, vikiwamo ukatili wa kijinsia na matumizi ya dawa za kulevya.

"Tumekuwa tukilaumu serikali kuhusu mmomonyoko wa maadili badala ya kuchukua hatua, sasa CHAUMA tunataka viongozi wetu watakaochaguliwa wawe wenye kujaribu kufanya na sio kuilalamikia serikali," alisema Njiku.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya chama hicho kimesimamisha wagombea zaidi ya 100 na kuwataka wananchi kuwachagua viongozi wa chama hicho, ili waweze kutekeleza sera hizo na kuwaletea maendeleo.

Katika hatua nyingine, chama hicho kimesema kimelazimika kuendesha kampeni zake kidigiti pamoja na kutumia kipaza sauti kupita mtaani, kutokana na changamoto ya ukosefu wa rasilimali fedha.

Alisema wagombea wao wanafanya kampeni kwa kutumia vipaza sauti kwa kuwafuata wananchi katika maeneo yao na kuelezea sera na mipango yao.

# Aomba kura ili kuwaondolea michango wananchi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MGOMBEA wa nafasi ya Uenyekiti Mtaa wa Kambarage Mjini Njombe, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Emmanuel Kayombo, amesema kilichomsukuma kugombea nafasi hiyo ni kwenda kuwaondolea adha ya michango wananchi.

Akinadi juzi kwa wananchi katika eneo la Kambarage Getini, Kayombo alisema wananchi wa mtaa huo wameteseka kwa miaka mingi na suala la michango ikiwamo malipo kwa ajili ya fomu mbalimbali pamoja na ujenzi wa miundombinu ya shule.

"Hakuna mtu atatozwa fedha pale ofisini kuja kuomba ajaziwe fomu kwa ajili ya kwenda kuchukua mkopo kwa ajili ya kufanya biashara, ndugu zangu mkinichagua nitapunguza michango kutoka 30,000 hadi 3,000," alisema Kayombo.

Kayombo alisema ili kuweze kupatikana maendeleo ya kweli ni lazima wananchi wa mtaa huo wakichague CHADEMA.

Katibu wa chama hicho, Kanda ya Kati, Emmanuel Masonga alisema, wananchi ndio wenye uamuzi wa maendeleo wanayoyataka katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

"Kila uamuzi unaofanywa juu ya mtaa wenu iwe ni hospitali, shule, barabara, kitu chochote, mtayafanya nyinyi wananchi, kwa sababu viongozi mtakayemchagua wanatakiwa kuwaongoza kwa kile mtakachokiamua nyinyi, sio kiongozi anakaa ofisini kwake anaamua juu ya michango yenu," alisema Masonga.

Wakazi wa Mtaa wa Kambarage Mjini Njombe akiwamo Veronika Mwalongo wanakiri kuwapo kwa michango mingi ambayo imekuwa kero katika mtaa wao, jambo ambalo linawasukuma kuchukua hatua katika kukabiliana na adha hiyo.

"Tutachagua kiongozi ambaye atatuletea maendeleo katika mtaa wetu wa Kambarage hususani upande wa majengo ya afya, kupunguza makali ya michango ya watoto shuleni na mingine," alisema Veronika.



## Waajiri wasisitizwa kuzingatia sheria ya utoaji wa mikataba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Khamis Suleiman Mwalim amewataka waajiri nchini kuwapatia mikataba wafanyakazi wao ili kutii matakwa ya kisheria.

Akifungua mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu Kamisheni ya Kazi katika Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mayugwani Zanzibar, Mwalim alisema, mikataba ni suala la sheria.

Alisisitiza kuwa waajiri kuwafanyisha kazi wafanyakazi wao bila mikataba ni kosa kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

"Kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar, mfanyakazi wa sekta yoyote ni lazima kupewa mkataba, kinyume na hilo ni kwenda kinyume na sheria hizo na ni kosa ambalo halikubaliki," alisema.

Mwalima alisema kuna wafanyakazi wengi wa sekta binafsi hawana mikataba na hawalipwi mishahara yao kwa mujibu wa sheria, lakini bado wanaendelea na kazi na hawatoi taarifa kwa kuogopa kufukuzwa.

Alisema kuna baadhi ya wafanyakazi hasa wa sekta binafsi wanapata matatizo mengi ikiwamo kukosa mikataba na kuwataka waandishi wa habari kushirikiana na kamisheni ya kazi kutoa elimu ya sheria za kazi kwa wafanyakazi na jamii.

Kamishna wa Kazi kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Rashid Khamis Othaman, alisema wamepata mafanikio makubwa ikiwamo kupanda kwa mishahara, kutoa mikataba ya ajira 37,455 kwa Unguja na Pemba.

Alisema mafanikio mengine ni pamoja na kusuluhisha na kutatua migogoro ya kazi 636 kati ya 743 ilipokewa na kusikiliza pamoja na kupatiwa ufumbuzi wa migogoro hiyo.

Aliwataka waandishi wa habari kuwa mabalozi wazuri wa kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kufanya kazi wakiwa na mikataba.

"Waandishi wa habari licha ya kuwa nyinyi ni wahanga wa hilo, lakini pia ni mabalozi wa kuwaelimisha wananchi kuhusu jambo hili," alisema Rashid.

Waandishi wa habari walioshiriki katika mafunzo hayo, walisema wanafanya kazi katika mazingira magumu ikiwamo kukosa mikataba na kulipwa mishahara kinyume na maelekezo yaliotolewa na serikali.

# Matukio ya udhalilishaji yapungua Zanzibar

**Na Rahma Sulleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya matukio ya udhalilishaji yamepungua kwa asilimia 0.7 kufikia matukio 147 mwezi wa Oktoba mwaka huu, kutoka matukio 148 kwa mwezi Septemba mwaka huu, visiwani Zanzibar.

Katika matukio hayo, matukio ya kutorosha, shambulio la aibu, kukashifu yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Oktoba.

Akitoa taarifa za takwimu za udhalilishaji kwa waandishi wa habari visiwani hapa, Asha Mussa Mahfoudh, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira alisema, katika matukio hayo waathirika walikuwa 147 ambapo wengi ni watoto, sawa na asilimia 83.0, wanawake asilimia 11.6 na wanaume asilimia 5.4.

Alisema matukio ya kubaka yalikuwa 53, kulawiti na kunajisi 11, kuingilia kinyume na maumbile matukio mawili, kutorosha 21, shambulio la kukashifu 31 na shambulio 29.

"Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 26.1 kufikia matukio 147 kwa mwezi wa Oktoba, mwaka huu kutoka matukio 199 kwa mwezi wa Oktoba, 2023," alisema.

Alisema matukio ya kubaka, kulawiti na kuingilia kinyume na maumbile na shambulio yamepungua kwa mwezi wa Oktoba, mwaka huu," alisema Mahfoudh.

Alisema Wilaya ya Magharibi B Unguja imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyingine ambapo ina matukio 37, sawa na asilimia 25.2 ikifuatia Wilaya ya Mjini ambapo yameripotiwa matukio 32, sawa na asilimia 21.8.

Alisema Wilaya ya Kusini Unguja imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio ambapo yameripotiwa manne, sawa na asilimia 2.7.

Alisema matukio 113 kati ya matukio 147 yaliyoripotiwa yanaendelea na upelelezi, sawa na asilimia 76.9, matukio 25 yapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, sawa na asilimia 17.0, moja limefungwa na polisi na matukio manane yapo mahakamani sawa na asilimia 5.4.

Katika hatua nyingine, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar) kimesisitiza umuhimu wa Jeshi la Polisi kuharakisha upelelezi wa kesi ya udhalilishaji ya mtoto wa miaka sita anayedaiwa kudhalilishwa na kuuliwa kikatili.

TAMWA kimetaka ushahidi muhimu ukusanywe ili kuwasilishwa mahakamani, kwa lengo la kuondoa hofu katika jamii na kuonesha kuwa sheria, haki, usalama na ustawi wa wanawake na watoto zinapewa kipaumbele.

Kwa mujibu wa taarifa ya TAMWA iliyosainiwa na Mkurugenzi wa chama hicho Zanzibar, Dk Mzuri Issa imetaka jamii pindi inapokuwa na ushahidi au fununu kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi au mamlaka husika, ili kukamilisha uchunguzi.

Chama hicho kimewataka wazazi na walezi kuchukua hatua madhubuti za kuwalinda watoto wao dhidi ya watu wenye nia mbaya, kufuatilia mienendo yao na kuhakikisha mazingira wanayoishi ni salama.

"Kuwapo ushirikiano wa familia, jamii na taasisi zinazohusika na ustawi wa watoto ni vyema kuzuia matukio ya ukatili na udhalilishaji katika jamii pamoja na kuhakikisha watoto wanalelewa katika mazingira yenye upendo na usalama," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za TAMWA Zanzibar tangu mwaka 2016, matukio 29 ya mauaji ya wanawake na watoto yameripotiwa (wanawake 24 na watoto watano), huku yaliyofikishwa Mahakama Kuu ya Zanzibar yakiwa ni machache.



Upanuzi wa Barabara ya Morogoro kwa njia sita ukiendelea katika eneo la Kimara Resort, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasisitizwa umuhimu wa amani kuchochea mapato zaidi ya utalii

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad amewataka wananchi kuendelea kuitunza amani iliyoko, kwani ndiyo kichocheo kikubwa cha utalii nchini.

Kamishna Hamad aliyasema hayo katika uzinduzi wa operesheni maalum ya kuzuia na kukabiliana na matukio ya uhalifu na ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani ambapo uzinduzi huo umefanyika Shehia ya Kwamtipura, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema sekta ya utalii ni muhimu katika kuchochea maendeleo makubwa nchini na inamgusa kila mmoja katika jamii, hivyo endapo nchi itakuwa haina amani, itachangia watalii kutokuja na kuathiri mapato ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea shughuli za kitalii.

Kamishna Hamad alisema kupitia uzinduzi wa Filamu ya Royal Tour iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan imeongeza watalii nchini.

Alsisitiza kuwa ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha amani inadumishwa ili kutoa fursa ya watalii hao kufanya utalii nchini.

Kamishna Hamad alisema madereva wa bodaboda wanapaswa kuwa sehemu ya kudumisha usalama na sio chanzo cha uhalifu.

Alisema kumekuwa na matukio kadhaa yanayohusisha madereva hao kufanya unyang'anyi, kusambaza dawa za kulevya na hata kusafirisha wahalifu kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Aliwaagiza masheha kupita nyumba kwa nyumba ili kuwabaini wahalifu na hatua za kisheria kuchukuliwa bila kumwonea mtu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Richard Mchomvu, alisema takribani watuhumiwa 50 walikamatwa katika operesheni ya kuzuia mapanga iliyozinduliwa mwezi Mei, mwaka huu, wanatumikia adhabu za vifungo jela na kuahidi kuendelea kuisimamia ili kuhakikisha wahalifu wanadhibitiwa.

# Funga kazi kwa vigogo wakihitimisha kampeni za uchaguzi serikali za mitaa

Inatoka Ukurasa 2

**VITUO VYAONGEZWA**

Mwenyekiti wa CHADEMA mkoani Shinyanga, Emmanuel Ntobi, amelalamikia ongezeko la vituo vya kupigia kura katika Manispaa ya Shinyanga bila wao kushirikishwa ili kuweka mawakala.

Alisema awali waliambiwa vituo vya kupigia kura vitakuwa 163, lakini jana jioni wakashtukizwa na kuambiwa vimeongezeka 122 na kufika 285, jambo ambalo wamelalamikia huenda ni maandalizi ya 'bao la mkono'.

Katibu wa CHADEMA, Kanda ya Victoria, Zakaria Obadi, alisema vituo tisa pia vimeongezwa katika kata ya Nyegezi jijini Mwanza tofauti na idadi ya mawakala waliowaandaa.

**AHAMIA CCM**

Mgombea Uenyekiti wa ACT Wazalendo katika Kijiji cha Igung'wa, Kata ya Kitwana, Kahama mkoani Shinyanga, William Nkwabi, ameandika barua ya kujitoa katika nafasi hiyo na kujiunga CCM.

Mgombea wa CHADEMA katika Mtaa wa Buswelu 'A' wilayani Ilemela, Mwanza, Pastory Apolinary, amedaiwa kupotelea kusikojulikana baada ya kupokea simu ikimtaka kwenda kuchukua mchango wa kampeni.

Nkwabi alisema ameamua kuandika barua hiyo baada ya kupimwa na daktari na kubaini kuwa anatakiwa kupumzisha mwili wake kutokana na umri alio nao kwa sasa, hivyo hawawezi kukimbizana na kampeni.

Alisema amefikia uamuzi huo bila kushawishiwa na mtu na akiwa na akili timamu, hivyo kwa sasa atakuwa mwananchi wa kawaida na kushiriki uchaguzi wa viongozi na wajumbe wa serikali ya kijiji kama walivyo wengine.

"Nitamuunga mkono mgombea wa CCM, ninawaomba wafuasi wangu wa ACT Wazalendo kuungana nami kumuunga mkono mgombea wa CCM. Kabla ya kujiunga na ACT Wazalendo, nilikuwa CCM," alisema.

Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Maalunga, Baraka Jilumbi alisema, mlango wa chama chao uko wazi kwa mtu yeyote anayetaka kujiunga.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Hezekiah Wenje, alisema: "Ilikuwa saa 7:00 mchana mgombea wetu akijiandaa na mkutano, mtu akampigia simu akamwambia ni mdau wa CHADEMA anataka niwape mchango kidogo katika kampeni. Akaenda kuonana na huyo mtu ndipo akapotea moja kwa moja mpaka jioni alikuwa hajaonekana."

Wenje alisema tayari taarifa imeshatolewa Jeshi la Polisi, huku wakiendelea kufuatilia mawasiliano ya mtu huyo aliyemwita.

Akizungumza kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilbrod Mutafungwa, alikanusha kuwa na taarifa za kutekwa kwa mgombea huyo, lakini akasema wanafuatilia kujua ukweli wa madai hayo.

**Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Hezekiah Wenje, alisema: "Ilikuwa saa 7:00 mchana mgombea wetu akijiandaa na mkutano, mtu akampigia simu akamwambia ni mdau wa CHADEMA anataka niwape mchango kidogo katika kampeni. Akaenda kuonana na huyo mtu ndipo akapotea moja kwa moja mpaka jioni alikuwa hajaonekana."**

**UVAMIZI OFISI CHADEMA**

Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, amelaani na kukemea vikali tukio la ofisi za chama hicho katika Kata ya Soweto, Manispaa ya Moshi, kuvamiwa na watu wasiojulikana, kupiga viongozi waliokuwamo, kuvunja vizimba vya chama hicho, Soweto na First & Last.

Akizungumza jana na waandishi wa Habari kabla ya mkutano wa kuhitimisha kampeni, Lema alisema: "Tunawaomba polisi, warudi katika kazi yao wawafuate na wafanye upelelezi kama ambavyo wanafanyaga upelelezi kutoka kwetu.

"Vitisho vinaathiri sana ustawi wa amani na maisha ya pamoja ya kijamii. Baada ya uchaguzi bado sisi ni ndugu, bado sisi ni majirani tutatibiwa hospitali moja, tutapanda daladala zile zile baada ya uchaguzi. Hii kutishana hii si ya kisiasa tu, inaingia kwenye maisha ya kijamii.

"Wamewatisha wagombea wetu kwamba, wasipojitoa watawafanyizia na baada yake wamejitoa. Wanawatisha viongozi wetu, wengine hawataki hata kutoka nje. Sasa hivi vitisho havitaishia katika uchaguzi, vitaendelea baada ya uchaguzi. Jeshi la Polisi fuatilieni vitisho tunavyofanyiwa."

Kwa mujibu wa Lema, kuna vitisho vimefanywa katika Kata ya Mabilioni, Halmashauri ya Wilaya ya Same, vingine vimefanywa katika Kata ya Miembeni, Mtaa wa Langoni, Manispaa ya Moshi, ambako mgombea amehama Moshi kabisa.

"Kule Soweto, Manispaa ya Moshi, nako wagombea wetu si mmoja, wametishiwa. Wale waliosimama imara ndio hili tukio la kuvamia ofisi limetokea.

"Tuna vitisho Siha, Kata ya Karansi na Kata ya Ngarenairobi. Tuna vitisho Vunjo, tuna vitisho tunavyo Rombo. Sasa kwa bahati mbaya tuna taarifa ya vitisho vingi usiku huu na kamatakamata ya vijana wa CHADEMA.

"Tunashauri kuwakamata haindoi ujasiri wa kuipenda nchi yao, hatujengi uzalengo kwa kuharibu imani ya watu kwenye nchi yao," alisema.

**VIJANA CCM**

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), Mohammed Kawaida, alizungumza na waandishi wa habari akisema uchaguzi huo usiwe wa kupuuza, bali iwe fursa muhimu kwa kila Mtanzania hasa vijana kuonesha dhamira ya kweli ya kuleta maendeleo endelevu kwa taifa.

Alisema Watanzania wote wana wajibu wa kuchagua viongozi waadilifu, wanaojali maslahi ya wananchi na wenye uwezo wa kusimamia maendeleo na kusisitiza kuwa ni muhimu Watanzania kuchagua viongozi ambao wanaona wanafaa katika kuleta maendeleo.

"Kuna sababu mbalimbali za msingi za kwa nini, wananchi wanapaswa kuiunga mkono CCM katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa ikiwamo suala la kuona mafanikio ya kiuchumi.

"Mengine ni ustawi wa jamii kupitia miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imetelezwa ikiwamo Reli ya Mwendokasi (SGR), Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), na uboreshaji wa bandari yamefungua fursa nyingi za ajira na kukuza uchumi wa ndani," alisema.

Aliongeza kuwa: "CCM ni chaguo bora kwa Watanzania kutokana na historia yake, mafanikio na sera zake zinazojikita katika ustawi wa kila raia ambako kimewezesha utoaji wa elimu bila malipo, afya, maji safi na salama, uwezeshaji wa vijana, wanawake, na wenye ulemavu huku kikitambua nafasi ya makundi yao katika maendeleo ya taifa."

Kawaida alisema katika uchaguzi huo ni muhimu kwa wananchi kuendelea kuichagua CCM ili kuhakikisha mabadiliko hayo yanaendelea, na miradi ya maendeleo inazidi kuwa na tija kwa jamii nzima.

Alisema chama hicho kinatambua mafanikio ya serikali katika ngazi zote za kitaifa, yanategemea ufanisi wa viongozi wake na kwamba, chama kimewekeza katika kuwaandaa na kuwajengea uwezo viongozi wake kupitia mafunzo ya uongozi na utendaji.

**POLISI KUSAMBAZWA**

Jeshi la Polisi nchini, kupitia taarifa yake iliyotolewa jana na Msemaji wake, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime, ilisema wananchi wataona askari polisi mtaani, nje ya vituo vya kupigia kura.

Alisema askari polisi hao watasambazwa kwa lengo la kuhakikisha usalama unakuwapo wakati wote wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa kila Mtanzania kuhakikisha anadumisha amani, utulivu, upendo na usalama kipindi chote cha kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo na baada ya uchaguzi.

"Kamwe usiwe chanzo cha uvunjifu wa amani, kwani hutaonewa muhali, lazima utachukuliwa hatua za kisheria.

"Kamwe tusiwape nafasi, wala kusikiliza au kufuata matamshi na vitendo vya viongozi au wafuasi wao ambayo lengo lake ni kutaka kuvuruga amani, utulivu na usalama wa nchi yetu," alisema Misime.

- **Imeandikwa na Godfrey Mushi (MOSHI), Romana Mallya, Jenifer Gilla, Gwamaka Alipipi,Maulid Mmbaga, Elizabeth Zaya, (DAR), Shaban Njia (KAHAMA), Vitus Audax (MWANZA), Judith Julius, (NGARA) na Marco Maduhu (SHINYANGA)**


## KUPOTEA KWA CHETI



**AMRI HASSANI SAID** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S3248/0125** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MFARANYIKA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019, Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/RUV/SON/4388/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDG. FRANK ONESMO MWASUMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki (Blue card) yenye namba za usajili **MC 942 DCC,** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu. TAARIFA YA POLISI:**PHQ/RUV/SON/7142/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRACE B MWASEGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0561/0025** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MONTFORT SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi **:PHQ/DAR/UBU/241645/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEWIS SAHA MCHARO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.456 CAB** aina ya **Toyota BREVIS .** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi; **MKO/RB/604/2024.**

**PUBLICATION SUMMONS**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**CIVIL CASE NO.27061/2024**

**SANDRU ABDUMARICK NDYANABO.........PLAINTIFF**

**VERSUS**

**CHINA JIANGXI INTERNATIONAL ECONOMIC & TECHNICAL COOPERATION LTD............1ST DEFENDANT**

**RAYMOND RICHARD @ URASSA...............2ND DEFENDANT**

**NOTICE OF HEARING**

**TO: RAYMOND RICHARD @ URASSA**

**TAKE NOTICE** that mentioned case has been set down for Hearing on the 02 day of DECEMBER, 2024 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. W. YONA – SRM. Your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 25 day of NOVEMBER, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

BUKOBA

# Mataifa yaonesha nia kujiunga BRICS

**KAZAN, Russia**

MATAIFA ya Amerika ya Kusini yakiwemo Bolivia, Colombia na Uturuki yameonesha nia ya kujiunga na Umoja wa Mataifa yanayochipukia Kiuchumi (BRICS), kama njia ya kujiimarisha kiuchumi, na kukuza ushirikiano wa kimataifa wenye haki zaidi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, akizungumza kabla ya mkutano wa kilele huko Kazan, alieleza namna BRICS ilivyyomuhimu katika mabadiliko ya uchumi wa kimataifa.

Alibainisha jinsi maeneo mapya ya ukuaji wa uchumi yalivyyotokea, hasa katika mataifa ya Ulaya na Asia-Pacific, na kwamba BRICS inafanya kazi tofauti na mataifa ya magharibi kama Umoja wa Ulaya (EU) ambazo hutunga maamuzi ambayo hayaendani na maslahi ya mataifa wanachama.

"BRICS, inahamasisha ushirikiano bila kuweka shinikizo lisilo la lazima kwa wanachama wake, jambo linalofanya kuwa chaguo bora," alisema Lavrov.

Aliongeza kwamba BRICS haina nia ya kushindana au kudhibiti nchi yoyote bali inataka kuongeza uwezo wa pamoja wa mataifa wanachama kupitia ushirikiano katika sekta mbalimbali kama biashara, mawasiliano, na teknolojia za kisasa.

Aidha, alieleza kwamba uwazi huo umesababisha ongezeko la hamu, hasa kutoka kwa nchi za Amerika Kusini, kutaka kujiunga na BRICS, na kwamba Brazil tayari ni moja ya wanachama waanzilishi.

Mtaalamu kutoka Amerika Kusini na Karibiani, Dk. Aparajita Pandey alisema: "Nchi zaidi zimeonesha hamu ya kuwa wanachama wa BRICS linaloendelea kuwa mbadala kwa mifumo ya magharibi inayotawala taasisi za kiuchumi za kimataifa."

Alisema kuwa mvuto wa BRICS kwa kanda hiyo unatokana na uwakilishi wake wa wengi duniani na uwezo wake wa kushughulikia mahitaji ya kiuchumi na maendeleo bila vikwazo vinavyowekwa na mifumo ya kifedha ya nchi za magharibi.

Hata hivyo, mojawapo ya nchi iliyoonesha nia ya kujiunga na BRICS ni Bolivia ambayo imeona ni fursa ya kuongeza ushiriki wake katika biashara ya kimataifa.



Zoezi la uokoaji likiendelea baada ya shambulizi la anga la Israel lililolenga jengo la makazi Lebanon, huku ikielezwa kuwa mahasimu hao wamekubaliana na masharti ya kusitisha vita. **PICHA: MTANDAO.**

# Trump azigeukia Canada, China na Mexico

## • Ni kuhusu kuongeza ushuru
## • Thamani za fedha nazo zashuka

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS mteule wa Marekani Donald Trump ameahidi ongezeko kubwa la ushuru kwa bidhaa zinazotoka Canada, China na Mexico kuanzia siku ya kwanza ya utawala wake, sera ambayo inaweza kuongeza kwa kasi gharama kwa wafanyabiashara wanaopeleka bidhaa nchini humo.

Trump alisema jana kuwa hatua hiyo itakuwa ya kulipiza kisasi kwa uhamiaji haramu na uhalifu wa dawa za kulevya unaovuka mpaka.

Alisema kuanzia Januari 20, mwakani kama mojawapo ya maagizo ya kwanza ya utendaji, atatia saini hati zote muhimu za kutoza ushuru wa asiliami 25 kwa Canada na Mexico kwa bidhaa zote zinazoingia Marekani.

"Ushuru huu utaendelea kutumika hadi wakati ambako dawa za kulevya, haswa Fentanyl, na wageni haramu wote wakomeshe uvamizi huu wa nchi yetu, na majirani wa Amerika wanaweza kutatua kwa urahisi shida hii ya muda mrefu," Trump alisema.

Aliongeza kuwa China itakabiliwa na ushuru wa juu kwa bidhaa zake kwa asilimia 10 juu ya ushuru wowote uliopo hadi itakapozuia mtiririko wa dawa haramu nchini Marekani.

"Nimekuwa na mazungumzo mengi na China kuhusu kiwango kikubwa cha dawa, haswa Fentanyl, kutumwa Amerika. Lakini bila mafanikio," Trump aliandika kupitia jukwaa la 'Truth Social'.

Aidha, alidai katika chapisho hilo kwamba maofisa wa China walimwahidi kuwa nchi hiyo itawanyonga wafanyabiashara wa dawa za kulevya waliopatikana wakiingiza dawa za kulevya nchini Marekani lakini hawakutekeleza hilo.

Akijibu hatua hiyo, Msemaji wa Ubalozi wa China Liu Pengyu, alisema nchi yake imekuwa katika mawasiliano na Marekani kuhusu operesheni za kukabiliana na dawa za kulevya na kwamba wazo la China kwa kujua kuruhusu vitangulizi vya fentanyl kuingia Marekani linakwenda kinyume kabisa na ukweli."

"Kuhusu suala la ushuru wa forodha wa Marekani kwa China, China inaamini kuwa ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara kati ya mataifa haya mawili una manufaa kwa pande zote. Hakuna atakayeshinda vita vya kibiashara au vita vya ushuru," Liu alisema katika taarifa yake.

Katika taarifa iliyotolewa kupitia ukurasa wa X maofisa wa Canada walijibu hatua hiyo wakisema kwamba nchi yao inaweka kipaumbele cha juu zaidi kwenye usalama wa mpaka na uadilifu wa mpaka wao wa pamoja ambayo ni muhimu kwa usambazaji wa nishati ya ndani ya Amerika.

"Bila shaka tutaendelea kujadili masuala haya na utawala unaokuja," Naibu Waziri Mkuu wa Canada Chrystia Freeland na Waziri wa Usalama wa Umma Dominic LeBlanc walisema katika taarifa hiyo.

**MABADILIKO YA SERA**

Ilielezwa kuwa ushuru huo ambao ni kama wa kuadhibu, ikiwa utapitishwa, unaweza kusababisha uharibifu kwenye minyororo ya usambazaji ya Amerika na viwanda vinavyotegemea bidhaa kutoka kwa washirika wa karibu wa biashara wa nchi hiyo.

Mtaalamu mkuu wa soko katika mipaka Karl Schamotta, alisema hatua zilizopendekezwa jana zinaweza kuathiri vibaya sekta kadhaa za kimkakati za kiviwanda za Amerika.

"Athari zitakazojitokeza ni kama kuongeza takriban dola bilioni 272 kwa mwaka kwa mizigo ya ushuru, pamoja na bei ya bidhaa, kuinua viwango vya riba, na kupunguza nguvu katika sekta ya kaya ambayo tayari iko katika hatari," alisema.

**FEDHA ZASHUKA**

Aidha, ilielezwa kuwa baada ya tangazo hilo, dola ya Canada ilishuka kwa asilimia 1.2 dhidi ya Marekani, na pesa ya Mexico ilishuka kwa asilimia mbili, huku Yuan ya Uchina, ingawa ilidhibitiwa na serikali, ilifanya biashara ya juu zaidi ya asiliamia 7.6 katika masoko ya nje ya nchi.

Ingawa wawekezaji waliamini kwamba ushuru unaweza hatimaye kuimarisha dola, masoko ya kifedha ya Amerika yalipata pigo, na kwamba ushuru wa ajabu ungeongeza gharama kwa Wamarekani kwa bidhaa za kila siku ambazo hapo awali zilivuka mpaka bila ushuru wowote wa kuagiza. Hata hivyo, ilielezwa kuwa mabadiliko hayo ya kushangaza yanaweza kudhoofisha ukuaji wa uchumi, haswa ikiwa watumiaji waliochoka na mfumuko wa bei wanatumia kidogo katika kukabiliana na gharama kubwa.

Ilielezwa kuwa hatima ya hisa ya Marekani, ambayo ilikuwa ya juu zaidi kabla ya tangazo la Trump, ilishuka kwa kiasi fulani hatima na kwamba bei za dhamana za hazina ya taifa hilo pia zilishuka.

**KINACHOAGIZWA**

Uagizaji mkuu wa Marekani kutoka Canada ni mafuta, ambayo yalifikia rekodi ya mapipa milioni 4.3 kwa siku mwezi Julai, kulingana na Utawala wa Taarifa za Nishati wa Marekani.

Pia kwa mujibu wa Comtrade ya Umoja wa Mataifa, Marekani inaagiza magari, mashine na bidhaa nyingine mbalimbali, plastiki na mbao kutoka Canada.

Kulingana na data ya biashara iliyotolewa na Idara ya Biashara mapema mwaka huu, Amerika inapata idadi kubwa ya magari na vipuri vyake vya magari kutoka Mexico, ambayo iliipita China kama msafirishaji mkuu wa Marekani mwaka 2023.

Mexico pia ni muuzaji mkuu wa vifaa vya kielektroniki, mashine, mafuta na vifaa vya macho, na kiasi kikubwa cha samani na pombe kwenda Marekani.

Pia Marekani inaagiza kiasi kikubwa cha vifaa vya kielektroniki kutoka China, pamoja na mashine, midoli, michezo, vifaa vya michezo, samani na plastiki.

Ilielezwa kuwa Trump alifanya kampeni ya kutumia ushuru kama kichocheo dhidi ya nchi za kigeni kama alivyofanya katika utawala wake wa kwanza kukuza viwanda vya ndani huku akiongeza mapato ya ushuru kulipia mapungufu makubwa ya mapato ambayo mpango wake wa kupunguza ushuru ungeunda.

## Pete Muungano kuanza kesho Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Muungano ya mchezo wa Pete 'Netball' yanatarajiwa kutimua vumbi kuanzia kesho Novemba 28 hadi Desemba 7, mwaka huu, nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa, alisema lengo la mashindano hayo ni kupata wachezaji watakaounda Timu ya Taifa.

Mwenyekiti huyo alisema yatashirikisha timu tisa za Tanzania Bara pamoja na sita kutoka visiwani Zanzibar ambazo zilishika nafasi ya kwanza mpaka ya tisa katika mashindano ya Ligi Daraja la Kwanza yaliyokuwa yamefanyika Agosti mwaka huu mkoani Arusha.

"Maandalizi kuelekea mashindano hayo yamekamilika kwa asilimia 99 mpaka sasa, kwani kila kitu kipo sawa tunasisitiza kila mchezaji kuongeze juhudi ya kufanya mazoezi," alisema Marwa.

Alisema miongoni mwa timu hizo zipo za Wanaume na Wanawake na kwamba timu zote zinatakiwa kuripoti Novemba 27, mwaka huu.

## Kuogelea Taifa wapongezwa

**Na Shufaa Lyimo**

VYAMA vya michezo nchini vimetakiwa kuiga mfano wa juhudi zinazofanywa na viongozi wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA).

Hayo yalisemwa juzi jioni na Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu, wakati akiipokea Timu ya Taifa ya Vijana ya Kuogelea iliyokuwa imetoka Bujumbura nchini Burundi kushiriki mashindano ya Afrika Kanda ya Tatu.

"Ninawapongeza viongozi wa Chama cha Kuogelea, kwani wamekuwa wakifanya maandalizi mazuri kabla na baada ya mashindano, kitu ambacho kisababisha wachezaji kupata makombe na medali nyingi," alisema Maguzu.

Aidha, aliwapongeza pia waogeleaji hao kutokana na juhudi waliyoifanya katika mashindano hayo ambayo yalishirikisha jumla ya nchi tano na wao kushika nafasi ya pili.

Kwa upande wa Nahodha wa timu hiyo, Collins Saliboko, alisema amefurahishwa na ushindi huo na kuahidi Watanzania kufanya vizuri zaidi kwenye michuano ijayo.

"Kwa niaba ya wachezaji wenzangu nimefurahishwa na ushindi tulioupata nchini Burundi tunaahidi kufanya makubwa zaidi kwenye mashindano yajayo," alisema Saliboko.

# MAFUNZO FC SASA YAKAA KILELENI LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Mafunzo FC imekalia usukani kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kuwafunga wapinzani wao Mwembe Makumbi City bao 1-0 katika mchezo wa kukamilisha mzunguko wa 12 wa ligi hiyo.

Mchezo huo ulichezwa juzi, Jumatatu katika Uwanja wa Mau A majira ya saa 10 alaisiri na kushuhudiwa na mashabiki wengi.

Kwa matokeo hayo Mafunzo imefikisha alama 26, ikifuatiwa na Mlandege FC yenye Alama 24 na nafasi ya tatu ikikaliwa na Malindi SC yenye alama 23 sawa na Mwembe Makumbi City ambayo ipo nafasi ya nne.

Katika mchezo huo wa juzi ulikuwa wa aina yake kwani ndio ulioamua kinara wa ligi hiyo kutokana na timu zote mbili kuwa na alana sawa kabla ya kushuka dimbani.

Bao pekee la Maafande wa Mafunzo liliwekwa wavuni na Issa Nassor ndani ya dakika saba za nyongeza kabla ya kukamilisha dakika 90 za mchezo huo.

Akizungumza baada ya kumalizika mchezo huo, Kocha wa Mafunzo FC, Sheha Khamis, aliwapongeza wachezaji wake kwa kujuhudi kubwa walizofanya na kufanikiwa kupata ushindi katika mchezo huo muhimu.

Alikiri kuwa mchezo huo ulikuwa mgumu kwa pande zote kuanzia uwanjani hadi jukwaani kwa mashabiki ambao wote walikuwa wakizifuatilia timu zao.

Alisema amefanikiwa lengo lake alilolitaka katika kuhakikisha timu hiyo inakaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

"Uliikuwa mchezo mgumu na wenye maamuzi nani akae kileleni mwa msimamo wa ligi, ila bahati imetuangukia kwetu, hivyo bado tunahitaji kufanya vizuri zaidi," alisema. Hata hivyo, aliwapongeza mashabiki wa timu zote kwa kuonesha hamasa ya juu katika mchezo huo na kusababisha kuwa na ushundani mkali.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo, akimkabidhi Kombe Nahodha wa timu ya Kamba ya Wanaume ya TPA, Mathias Iyon, katika mashindano ya SHIMMUTA yaliyomalizika jijini Tanga mwishoni mwa wiki ambapo TPA waliibuka mabingwa wa jumla. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TPA bingwa mashindano ya SHIMMUTA 2024

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imetwaa Ubingwa wa Jumla wa Mashindano ya Mashirika ya Umma, Kampuni na Taasisi Binafasi nchini (SHIMMUTA), kwa mwaka 2024 katika michuano iliyofanyika jijini Tanga.

Katika mashindano hayo ambayo yalifungwa rasmi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo, yalishuhudiwa timu nne za TPA zikitawazwa mabingwa rasmi wa mashindano hayo.

Timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa mashindano hayo ni ya mpira wa Kikapu ya TPA ambayo iliichabanga NSSF kwa jumla ya vikapu 57 - 45 katika mchezo wake wa fainali. Ubingwa huo ni wanne mfululizo kwa TPA.

Katika mchezo wa mpira wa pete 'Netball', timu ya TPA ilitwaa ubingwa huo kwa kuifunga TMDA kwa magoli 53 - 43 kwenye mchezo wa fainali wa mashindano hayo. Huo ukiwa ni ushindi wanne mfululizo kwa timu hiyo ya TPA kutawazwa mabingwa wa mashindano hayo kwa mchezo huo.

Kwa upande wa mpira wa Kamba, timu ya wanawake na wanaume zote za TPA, zilishinda michezo yao ya fainali, ambapo timu ya wanawake iliibuka kidedea dhidi ya TPDC, huku wanaume wakishinda dhidi ya TBS. Timu zote mbili za TPA zimetwaa ubingwa huo kwa mara ya tatu mfululizo.

Na kwa upande wa mchezo wa riadha, timu ya TPA ilishinda katika mbio za mita 200 na kujinyakulia medali za dhahabu, huku katika mikimbio ya wazee ya mita 100, timu ya TPA pia iliibuka kidedea kwa kupata ushindi wa pili na kujinyakulia medali ya fedha.

Katika michezo ya jadi, timu ya TPA haikuondoka mikono mitupu kwani Mwanamama Celine Simon alionesha umahiri wake kwa kuibuka mshindi wa tatu katika mchezo huo wa kusogeza kete yaani 'draft'.

Kutokana na ubingwa huo, timu za TPA zimeibuka mshindi wa jumla kwa mara ya pili mfululizo. Mara ya kwanza kuwa mshindi wa jumla ni mashindano ya mwaka 2023 yaliyofanyika jijini Dodoma. Katika mashindano yaliyofanyika jijini tanga mwaka 2024, jumla ya timu 96 kutoka taasisi za umma na binfasi zilishiriki.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**AMORIM AMTAKA AIT-NOURI**
KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, anatamani kumsajili winga wa Wolves na Algeria, Rayan Ait-Nouri mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun)***

**NKUNKU PIA ATAKIWA**
MANCHESTER United pia wanavutiwa na Christopher Nkunku wa Chelsea, lakini wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Borussia Dortmund kwa mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27. ***(TeamTalks)***

**SEMENYO AWINDWA**
KLABU ya Newcastle United inavutiwa na mshambuliaji wa Bournemouth, Antoine Semenyo mwenye umri wa miaka 24, lakini hawana uwezo wa kumnunua Januari hadi pale wachezaji wengine watakapoondoka. ***(Sky Sports)***

**FERGUSON KWENYE RADA**
FULHAM na Leicester wapo kwenye mbio moja kumwania mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, 20. ***(Football Insider)***

**DYCHE UHAKIKA EVERTON**
KOCHA wa Everton, Sean Dyche, anaungwa mkono kikamilifu na mmiliki wa sasa, Farhad Moshiri na ataendelea kuisimamia klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

**QUENDA AULIZIWA UNITED**
MANCHESTER United wameulizia kuhusu winga wa Sporting mwenye umri wa miaka 17, Geovany Quenda, ambaye thamani yake ni euro milioni 60. ***(A Bola)***

**CALVERT-LEWIN AGOMBEWA**
AC Milan wako tayari kushindana na Newcastle United kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Everton mwenye umri wa miaka 27, Dominic Calvert-Lewin, wakati Real Madrid wanafikiria kumnunua mlinzi wa Toffees, Jarrad Branthwaite, 22. ***(Teamtalk)***

**HAALAND KUSAINI TENA**
KLABU ya Manchester City ina imani kuwa mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 24, atamfuata Kocha wa Pep Guardiola kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Give Me Sport)***

**GYOKERES AKOMALIWA BARCA**
BARCELONA inatazamia dili la euro milioni 70 la kumnunua mshambuliaji wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 26, Viktor Gyokeres. ***(Sport)***

**MURRAY LULU BRIGHTON**
KLABU ya Brighton inatarajia kumnunua winga wa Cork City, Matthew Murray mwenye umri wa miaka 18 kwenye majaribio. ***(Irish Mirror)***

**MILAN KUJIUNGA JUVENTUS**
MLINZI wa PSG na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kujiunga na Juventus katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Foot Mercato).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE: SIJUI KAMA NITABAKI TENA MAN CITY

●●●Mwanzoni mwa msimu, nilijua mazungumzo yangefanyika, lakini jeraha likatokea, hivyo...

**MANCHESTER, England**

KEVIN De Bruyne amekiri kuwa hajui kama huu utakuwa msimu wake wa mwisho Manchester City na kufichua kuwa alisimamisha mazungumzo ya mkataba mpya baada ya kupata jeraha ambalo limemweka nje kwa miezi miwili iliyopita.

Mkataba wa De Bruyne unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Alisema alikuwa na mazungumzo na klabu katika msimu wa majira ya joto, lakini sasa analenga tu kupona vizuri.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, hajaanza mchezo wowote kwa Man City tangu Septemba 18, lakini jana Jumanne alitarajiwa kurejea dhidi ya Feyenoord kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwa kweli sijui," alisema De Bruyne akiwaambia waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu mustakabali wake.

"Mwanzoni mwa msimu, nilijua mazungumzo yangefanyika, lakini jeraha likatokea kwenye mchezo dhidi ya Brentford. Ilikusudiwa kuwa siku kadhaa na kisha ikawa wiki nane hadi tisa.

"Nilifanya mazungumzo katika majira ya joto, lakini baadaye nilipata jeraha kwa hiyo sikuwa sawa kuzungumzia hilo. Ninahitaji kurejea uwanjani na kuwa katika ubora wangu. Hakuna haraka, sijisikii vizuri, sina wasiwasi."

De Bruyne yuko katika msimu wake wa 10 ndani ya City na amekuwa akihusishwa na kuhamia Ligi Kuu ya Saudi Arabia na Ligi ya Kuu ya Soka ya Marekani katika Klabu ya San Diego FC.

Pep Guardiola pia alikuwa anatarajiwa kumalizika kwa mkataba wake msimu wa majira ya joto kabla ya kusaini mkataba wa nyongeza wa miaka miwili.

Na De Bruyne amesema kubakia kwa Guardiola kunaweza kuchochea uamuzi wake mwenyewe baada ya kushinda mataji sita ya Ligi Kuu England pamoja.

"Naweza kubaki," alisema De Bruyne.

"Najua mustakabali una nini, si lazima niongee na Pep kuhusu kile kinachotokea siku za usoni, kama kutakuwa na kocha mpya, lazima uzungumze.

"Labda Pep akabadilisha mawazo yake na kusema asante Kevin ni wakati wa kuondoka, lakini najua jinsi anavyofanya kazi na timu na wachezaji kwa hiyo hilo si jambo geni kwangu."

# Yamal kurejea dimbani Jumamosi



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, amefichua kwamba, Lamine Yamal anatarajia kupatikana Jumamosi wiki hii.

Nyota huyo aliumia kifundo cha mguu wa kulia kuelekea mwisho wa ushindi wa Barcelona wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Red Star mwanzoni mwa Novemba.

Yamal alilazimika kujiondoa kwenye kikosi cha Hispania kwa mwezi wa pili mfululizo na amekaa nje mechi mbili za mwisho za Barcelona - ambazo zote zimeifanya klabu hiyo kupoteza pointi.

Yamal alikosa kwenye sare ya 2-2 ya Barcelona dhidi ya Celta Vigo Jumamosi usiku, lakini Flick ana matumaini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, atarejea kikosini wikendi ijayo.

Akizungumza na vyombo vya habari kabla ya mechi ya Barcelona ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Brest ya Ufaransa jana Jumanne, Flick alisema: "Nadhani huu unaweza kuwa mchezo wa mwisho atakaoukosa. Jumamosi anaweza kuwa chaguo kutoka kwenye benchi."

Miamba hiyo ya Katalunya wameshinda mechi 14 kati ya 15.

Beki mkongwe wa kati Inigo Martinez aliulizwa kuhusu mchango wa Yamal katika mkutano huo na waandishi wa habari na akasema: "Tunajua jinsi alivyo muhimu, sitakataa hilo.

"Anaifanya safu ya ulinzi ya mpinzani kurudi nyuma. Anazua hofu kubwa. Yeye ni muhimu, lakini hiyo haimaanishi kwamba yeyote atakayechukua nafasi yake hafai.

"Kila anayekuja anajaribu kujitoa kwa asilimia 100 au 200. Lamine ni Lamine, hatunaye kwa sasa na hiyo haimaanishi kwamba kwa sababu hayupo hatutashinda. Tunapaswa kuzingatia tulio nao.

# Vinicius nje mwezi mmoja



**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid imethibitisha kuwa Vinicius Junior atahitaji muda wa kukaa nje ya uwanja baada ya kupata jeraha la misuli ya paja.

Vinicius alicheza dakika zote 90 za ushindi wa 3-0 Jumapili ugenini dhidi ya Leganes na hakuonekana kuonesha dalili zozote za kuumia wakati wa mchezo huo, ingawa ripoti za ndani zinasema Mbrazil huyo aliripoti tatizo kwenye chumba cha kubadilishia nguo baada ya filimbi ya mwisho.

"Vinicius amegundulika kuwa na jeraha la misuli ya paja", ilisema taarifa ya Real Madrid huku wakishindwa kutoa ratiba ya lini atarudi dimbani.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, Vinicius anatarajiwa kukosa kucheza kwa takriban mwezi mmoja, jambo ambalo, kwa kuzingatia mapumziko ya msimu wa baridi wa LaLiga, inamaanisha kwamba hatarejea kabla ya mwisho wa mwaka huu wa kalenda.

Jeraha hilo linakuja kama pigo kubwa kwa Madrid, ambao wanapigania kuweka sawa kampeni yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakikabiliana na Liverpool leo Jumatano.

Madrid tayari wamepoteza michezo miwili kati ya minne ya kwanza katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Liverpool wakiwa wamekaa kileleni mwa msimamo.

Kikosi cha Carlo Ancelotti kilitoa matokeo bora zaidi ya msimu mwishoni mwa juma baada ya mbinu iliyowahusisha Vinicius na Kylian Mbappe. Wawili hao hawakucheza vizuri kabla ya kubadilishana nafasi dhidi ya Leganes, Vinicius akianzia kama mshambuliaji wa kati na Mbappe akicheza winga ya kushoto.



# MOURINHO: RONALDO KUJA FENERBAHCE LABDA KUNYWA CHAI TU

**ISTANBUL, Uturuki**

KOCHA wa Fenerbahce, Jose Mourinho, amekanusha kwa msisitizo na kuziita tetesi za kipuuzi zinazomhusisha yeye kuungana na Cristiano Ronaldo kwenye Ligi Kuu ya Uturuki.

Kocha huyo raia wa Ureno aliteuliwa kuinoa Fenerbahce majira ya joto baada ya kutimuliwa na AS Roma.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kuungana tena na Ronaldo baada ya tetesi kuibuka atajiunga naye Uturuki, Mourinho alitumia sekunde nane kujibu: "Habari kuhusu Cristiano Ronaldo kuja Fenerbahce ni za kipuuzi."

Ronaldo alitumia misimu mitatu kuichezea Real Madrid akiwa na Mourinho kati ya 2010 na 2013. Fowadi huyo mahiri alikuwa kwenye kilele chake, akifunga mabao 168 katika mechi 164 katika kipindi hicho, ingawa Madrid walishinda Copa del Rey na La Liga pekee wakati wa utawala wa Barcelona.

Anapokaribia kufikisha umri wa miaka 40, Ronaldo hajaonesha dalili zozote za kukaribia kustaafu.

Mshambuliaji huyo wa Al Nassr amedokeza kwamba bado anaweza kucheza ifikapo mwaka 2027.

Hata hivyo, mkataba wake na timu hiyo ya Saudi Pro League unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na kuwafanya baadhi ya watu kudokeza kwamba huenda tayari anapanga uhamisho wake mwingine.

Mourinho alikuwa mwepesi kusisitiza kwamba mwisho wa Ronaldo hautakuwa jijini Istanbul.

"Cristiano anaweza kuja Istanbul kula chakula kwa sababu ni katikati ya barabara kati ya Saudi na Ureno," alisema kocha huyo.

"Au labda atakuja kumuona rafiki yake wa zamani Jose, tunaweza kula hotelini kwangu."

Wareno hao wawili wana wakala mmoja mwenye ushawishi mkubwa, Jorge Mendes.

# GAMONDI ATAJWA KUCHUKUA NAFASI YA AUSSEMS SINGIDA BS

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Klabu ya Singida Black Stars kumsimamisha kazi Kocha Mkuu, Patrick Aussems na Msaidizi wake, Denis Kitambi, habari zinasema huenda Kocha Mkuu wa zamani wa Yanga, Miguel Gamondi, akachukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho.

Klabu hiyo juzi ilitoa taarifa ya kuwasimamisha makocha hao kwa kile ilichodai ni mwenendo usioridhisha katika michezo mitatu mfululizo, licha ya jitihada zote kufanyika kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo kuwapatia benchi la ufundi kila wanachohitaji.

Klabu hiyo imesema kuwa maamuzi hayo yamefanywa na Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo iliyochaguliwa hivi karibuni.

"Kipindi chote ambacho Aussems na Kitambi hawatakuwa kazini, kikosi kitakuwa chini ya Mkurugenzi wa Ufundi, Ramadhani Nsanzurwimo kama kocha mkuu, huku msaidizi wake akiwa Muhibu Kanu.

Singida imefanya maamuzi hayo, baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tabora United katika mchezo uliochezwa juzi, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, ikiwa ni moja kati ya mechi tatu zinazowahukumu makocha hao. Oktoba 30 ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Yanga huku Novemva 2, mwaka huu, ikitoka suluhu dhidi ya Coastal Union.

Akizungumzia hilo, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hussein Massanza, alisema, si kawaida ya timu yao kwa msimu huu kucheza michezo mitatu bila ushindi, kwao hawataki uzoeleke na usionekana wa kawaida kwani Singida pia ina kikosi bora kama timu zingine kubwa zinazowania ubingwa.

"Ukiangalia timu tunazotoa nazo sare ukazilinganisha na Singida Black Stars, tumezipita kiwango kwa kiasi kikubwa, kwa maana hii timu inaonesha inaanza dalili za kushuka kiwango, Bodi ya Wakurugenzi ikaona ichukue hatua hizi ambazo ni za mwanzo, huko mbele tutaangalia nini kitaendelea," alisema.

Hata hivyo, habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema klabu hiyo imekuwa na mazungumzo na Gamondi aliyetimuliwa hivi karibuni na Yanga, ambaye inasemekana bado yupo nchini.

Taarifa zinasema huenda akapewa mkataba wa miaka miwili na anaweza kutambulishwa wakati wowote ule mambo yatakapokamilika.

Akizungumzia hilo, Massanza alisema bado halijafika mezani kwake, analofahamu kwa sasa ni kwamba makocha hao wamesimamishwa.

"Ieleweke hatujawafukuza makocha wetu bado wapo, ila kama tutalazimika kuachana nao moja kwa moja makocha wetu na kulazimika kutafuta wengine, tutayazungumza kama tulivyotoa taarifa hizi," alisema Massanza.

Timu hiyo inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 24 kwa michezo 11 iliyocheza.

## TUUJAZE UWANJA...




Mashabiki wa Simba wakihamasishana kununua tiketi Mbagala, Dar es Salaam jana, kuelekea mechi yao ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa 10 alasiri. **MPIGAPICHA WETU**

# Tanesco, Dar City zaanza 'First League' kwa kishindo

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU za Tanesco na Dar City, juzi zilianza vema michuano ya Ligi Daraja la Pili ‚First League' msimu wa 2024/25, kusaka timu zitakazopanda Ligi ya Championship msimu ujao, baada ya kushinda michezo yao ya ufunguzi.

Tanesco, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro, ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alliance FC, ukiwa ni mchezo wa Kundi B, huku Dar City, ikitoa kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya African Lyon, mechi iliyochezwa Uwanja wa Manungu, Complex uliopo Turiani, Morogoro, huo ukiwa ni mchezo wa Kundi A.

Nyumbu FC, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Hausing FC, huku Tunduru Korosho na Moro Kids zikianza ligi hiyo kwa suluhu, mechi ikipigwa, Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Jana kwenye Uwanja wa Mabatini, ulitarajiwa kucheza mchezo mwingine kati ya Magnet FC dhidi ya Pan African ambayo itacheza ligi hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kuteremka kutoka Ligi ya Championship msimu uliopita.

Ligi hiyo inazishirikisha jumla ya timu 16 zilizogawanywa kwenye makundi mawili, Kundi A likiwa na timu za Nyumbu FC, Dar City, Moro Kids, Tunduru Korosho, Magnet FC, Pan African, Hausing na African Lyon.

Kundi B linazishirikisha timu za Tanesco FC, Copco FC, Gunners FC, Mapinduzi FC, Rhino Rangers, Ruvu Shooting, TRA FC na Alliance FC.

Mshindi wa wanne wa kila kundi atafuzu kucheza hatua ya nane bora ambapo ligi hiyo itawapata washindi wawili watakaopanda kwenda Ligi ya Championship, huku pia zikichezwa mechi za mchujo kwa ajili ya kusaka timu nyingine moja itakayoungana nayo.

## Kocha Fadlu: Tutashambulia mwanzo mwisho leo

INATOKA UK. 24

tayari na tumeridhika na maandalizi, najua tuko kwenye kundi gumu, lakini tumejipanga kuanza vema," alisema.

Naye, Che Malone Fondoh, aliyezungumza kwa upande wa wachezaji, alisema wamejiandaa vema kuwapa wanachama, mashabiki wa Simba na Watanzania kwa ujumla furaha ya ushindi na mchezo safi.

"Sisi kama wachezaji tuko tayari, tuna imani kwa maandalizi tuliyoyafanya, hivyo tutafanya kila linalowezekana ili kupata ushindi wa kwanza nyumbani," alisema beki huyo wa kati raia wa Cameroon.

Mara ya mwisho Simba kucheza hatua ya makundi Kombe la Shirikisho ilikuwa ni msimu wa 2022, ilipofika hatua ya robo fainali na kutolewa na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa nchini, Aprili 17, 2022, Simba ilishinda bao 1-0, lakini ilifungwa pia bao 1-0 katika mchezo wa marudiano, Sauzi, Aprili 24, 2022, zikalazimika kupigiana mikwaju ya penalti, Simba ikatolewa kwa matuta 4-3.

Simba iko Kundi A, pamoja na timu za Bravo do Maquis, CS Sfaxien ya Tunisia na CS Costantine ya Algeria.

## Ramovic abatizwa kwa moto Yanga

INATOKA UK. 24

Stephane Aziz Ki, ambaye alimwekea kwenye njia Dube, lakini hakufanikiwa kuuweka kwenye himaya yake.

Dakika mbili baadaye Nickson Kibabage alimzidi mbio Al Tayeb Abadallah, lakini akiwa kwenye nafasi nzuri ya kukwamisha wavuni, mguu wake ulipata kigugumizi na beki huyo akafanikiwa kumuwahi kumbabatiza mpira miguuni ukatoka kona ambayo haikuzaa matunda.

Straika hatari wa Al Hilal, ambaye aliifunga Yanga katika michezo yote miwili mwaka 2022, Mohamed Abdelrahman, nusura afunge bao dakika ya 34, alipowahadaa mabeki, waliompa nafasi ya kupiga shuti nje kidogo ya eneo la hatari ambao ulimpita kipa Djigui Diarra, lakini ukatoka sentimeta chache langoni.

Diarra alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika mbili kabla ya kwenda mapumziko, alipojitosa na kupangua krosi ya Adama Coulibaly iliyokuwa inakwenda kichwani mwa Abdelrahman na kuiweka salama timu yake.

Nafasi ambazo Yanga itabidi izijutie ni za dakika ya 55, ambapo krosi ya Nickson Kibabage iliunganishwa kwa ustadi kwa kichwa cha kudundisha na Aziz Ki, wakati kila mmoja akidhania mpira unakwenda wavuni, Fofana aliruka juu na kupiga ngumi ukatoka juu ya lango.

Musonda alikaribia kuifungia Yanga bao dakika ya 77, akiwa amepata pasi ya juu kutoka kwa Aziz Ki, lakini mpira ukagonga nguzo ya juu na kurejea uwanjani.

Michezo
Nipa
Jumatano Novemba 27, 2024

## De Bruyne: Sijui kama nitabaki Man City
UKURASA 21





# RAMOVIC ABATIZWA KWA MOTO YANGA

Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube, akijaribu kufunga, lakini kipa wa Al Hilal, Issa Fofana, akawa makini kufuta hatari hiyo, kwenye mechi ya kwanza ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

### Al Hilal yamfunza soka, mabingwa hao wa Bara sasa waburuza mkia Kundi A, Siku ya Dude yageuka...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA imepoteza mechi ya tatu mfululizo baada ya jana kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal Omdurman ya Sudan, katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kundi A.

Ikicheza mechi ya kwanza chini ya Kocha mpya, Sead Ramovic, aliyechukua mikoba ya Miguel Gamondi aliyesitishiwa mkataba, Yanga, alikaribishwa kwa kipigo hicho ambacho unaweza kukiita ni sawa na ‚kubatizwa kwa moto' mbele ya maelfu ya mashabiki wa timu hiyo katika Uwanja wa Mkapa.

Hicho kinakuwa ni kipigo cha tatu mfululizo kwa Yanga, ambapo awali ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Novemba 2, mwaka huu na mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, Novemba 7, mwaka huu, mechi zote zikiwa ni za Ligi Kuu zilizochezwa, Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Mabao ya Al Hilal ambayo inacheza Ligi Kuu nchini Mauritania badala ya nchini kwao Sudan ambako kuna vita ya wenyewe kwa wenyewe, yote yalifungwa kipindi cha pili na winga wa kulia, raia wa Mali, Adama Coulibaly dakika ya 63 na Msudan, Yasser Muzammil aliyepachika bao dakika ya 90.

Bao la kwanza lilitokana na mpira mrefu uliopigwa kwa mfungaji ambaye alikuwa akikimbizana na Ibrahim Hamad ‚Bacca', aliyetaka kutumia nguvu zaidi kuliko akili kumdhibiti winga huyo mjanja, hivyo alimkwepa hali iliyomfanya beki huyo wa Kimataifa wa Tanzania, kuanguka.

Kitendo cha kuanguka kilimpa nafasi winga huyo kuumiliki mpira bila bugudha akiwa kwenye wingi ya kulia kwenye ‚engo' ngumu, alipiga shuti la kiufundi kwa mguu wa kushoto, lililompita Djigui Diarra katikati ya miguu na kujaa wavuni.

Muzammil, alifunga bao lake pia kwa mguu wa kushoto, akitumia makosa ya mabeki wa Yanga ambao wote walikuwa wamepanda mbele kwenda kusaidia mashambulizi ya mpira wa kona, lakini uliokolewa na mabeki wa Al Hilal na kupigwa mpira mrefu ambao uliomkuta mfungaji huyo aliyeingia kipindi cha pili, hivyo alikuwa bado na pumzi kuliko mabeki wa Yanga, akatoka nao katikati ya uwanja na kuingia ndani ya eneo la hatari, kabla ya kuupachika wavuni, akimwacha Diarra akiruka bila mafanikio.

Licha ya Yanga kufanya mabadiliko katikati ya kipindi cha pili, ikiwatoa Duke Abuya na Maxi Nzengeli, na kuwaingiza Wazambia Clatous Chama na Kennedy Musonda, bado hawakuweza kuipenya ngome ya Al Hilal, ikiongozwa na El Hadj Kane iliyokuwa ngumu kupenyeka, huku kipa Issa Fofana, akiwa mwiba mchungu kwa washambuliaji wa Yanga.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inaburuza mkia katika Kundi A, kutokana na TP Mazembe ya DR Congo kulazimishwa suluhu nyumbani jana na MC Alger ya Algeria.

Kipindi cha kwanza mechi ilianza taratibu, ilipotimu dakika ya saba, Nzengeli aliambaa kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi ambayo ilikosa muunganishaji, huku Al Hilal ikijibu shambulio dakika tatu baadaye lililofanywa na Jean Claude, alipowatoka wachezaji wa Yanga kwenye wingi ya kulia, lakini krosi yake ilipaa juu ya lango.

Prince Dube ambaye mechi Yanga waliitangazwa kuwa maalum kwa ajili yake, angeweza kuipatia Yanga bao dakika ya nane ya mchezo, lakini aliumiliki vibaya mpira ukamzidi kasi, kabla ya kuwahiwa na kipa Issa Fofana.

Ilikuwa kazi nzuri ilioanzishwa na Mudathir Yahaya, aliyempenyezea,

INAENDELEA UK. 23

## Kocha Fadlu: Tutashambulia mwanzo mwisho leo

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Simba, leo jioni itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mchezo wa kwanza hatua ya makundi dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, huku Kocha Mkuu, Fadlu Davids, akisema hawatowaonea aibu wapinzani wao kuwashambulia kwa nguvu watakapokuwa na mpira.

Akizungumza kuelekea kwenye mchezo huo, utakaopigwa saa 10:00 jioni, kocha huyo alisema watawaheshimu wapinzani wao pale tu ambapo watakapokuwa hawana mpira miguuni, lakini wakiupata hawatowaonea aibu, badala yake watawashambulia kwa nguvu kwani wamedhamiria kupata ushindi wa kwanza ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kufuzu robo fainali kutoka Kundi A.

"Nimewaangalia wapinzani wetu, ni timu nzuri, ngumu yenye wachezaji wenye fiziki kubwa na baadhi yao ni wazuri nawajua kwa majina, wanapenda kucheza na washambuliaji wawili, tutawaheshimu tukiwa hatuna mpira, lakini tukiupata hatutawaonea aibu, tutawashambulia.

"Wachezaji wangu wanalijua hilo na wanajua michuano hii ni tofauti na Ligi Kuu, nadhani walipata kionjo katika mechi ya mtoano dhidi ya Al Ahli Tripoli," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Fadlu alisema wakati wa maandalizi ya mchezo wa leo, alikuwa na kazi ya kuinoa safu ya ushambuliaji, lakini pia walikuwa na sehemu ya mazoezi ya kupiga mikwaju ya faulo ambayo pia inaweza kuwasaidia kupata mabao katika mchezo huo.

"Maandalizi yamekwenda vizuri tangu tulipotoka Mwanza kucheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Pamba Jiji.

Mechi ile imenisaidia kujua baadhi ya vitu ambavyo nilihitaji kurekebisha na nimefanya hivyo. Tumefanya mazoezi ya kushambulia, na mengine ya mikwaju ya faulo, nafikiri kwa sasa tuko

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >